# Maombi kutoka kwenye Qur'ani na Sunna

Mtunzi

**Muhitaji kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu Daktari Said ibn Ally ibn Wahf Al-qahtaani**

شركاء التنفيذ:

دار الإسلام جمعية الربوة رواد الترجمة المحتوى الإسلامي

يتاح طباعة هذا الإصدار ونشره بأي وسيلة مع الالتزام بالإشارة إلى المصدر وعدم التغيير في النص.


Telephone: +966114454900

ceo@rabwah.sa

P.O.BOX: 29465

RIYADH: 11557

www.islamhouse.com

# Maombi kutoka kwenye Qur'ani na Sunna

﴿وَلِلَّهِ ٱلۡأَسۡمَآءُ ٱلۡحُسۡنَىٰ فَٱدۡعُوهُ بِهَاۖ وَذَرُواْ ٱلَّذِينَ يُلۡحِدُونَ فِيٓ أَسۡمَٰٓئِهِۦۚ سَيُجۡزَوۡنَ مَا كَانُواْ يَعۡمَلُونَ١٨٠﴾ [الأعراف: 180]

[1]"Na Mwenyezi Mungu ana majina mazuri basi muombeni kwayo na waacheni wale ambao wanaoharibu utakatifu wa majina yake hivi karibu watalipwa kwa yale waliyokuwa wakifanya"

[1] Suratu Al-Araafu: 180.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Allahu** | **Wa mwanzo** | **Wa mwisho** | **Hakuna yeyote aliye Juu yake** | **Aliye Karibu na viumbe wake kuliko chochote kile** |
| **Aliye juu** | **Wa Juu** | **Mtukufu Aliye juu** | **Aliye Mkuu** | **Wa Kuheshimiwa** |
| **Aliye Mkuu** | **Mwenye kusikia** | **Mwenye kuona** | **Aliye Mjuzi** | **Mjuzi wa Mambo yaliyofichikana** |
| **Msifiwa zaidi na waja wake** | **Mwenye Nguvu asiyeshindwa** | **Muweza** | **Mwenye uwezo wa kila kitu** | **Mwenye Nguvu** |
| **Aliye Madhubuti** | **Aliye jitosheleza** | **Mwenye Hekima** | **Mpole** | **Msamehevu** |
| **Mfuta Mdhambi** | **Mwingi wa Kufuta madhambi** | **Mwingi wa kukubali Msamaha** | **Msimamizi** | **Mwenye kushuhudia mambo ya waja** |
| **Mwenye Kuhifadhi** | **Mpole juu vitendo vya waja** | **Aliye karibu** | **Mwenye Kujibu** | **Mwenye kupenda** |
| **Mwingi wa kushukuru** | **Mwenye kushukuru** | **Mtukufu** | **Mkusudiwa** | **Mtenza nguvu** |
| **Mwenye nguvu juu ya kila kitu** | **Anaye fanya analolitaka** | **Mwenye kuhesabu** | **Muongozaji** | **Mwenye kuhukumu** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Aliye Takasika | Mwenye Amani | Mwenye wema | Mpaji Mkuu | Mwingi wa Rehema |
| Mwenye kurehemu | Mtukufu | Mwingi wa Ukarimu | Mpole | Mwingi wa Kufungua |
| Mtoaji wa Riziki | Aliye Hai Uhai uliokamilika | Msimamia kila jambo | Mlezi wa kila kitu | Mwenye Ufalme |
| Mwenye Utukufu | Aliye Mmoja wa Pekee | Mkubwa Mwenye kutakabari | Muumbaji | Mwingi wa Uumbaji |
| Mtia Sura | Mtengenezaji | Mwenye kuwasadikisha mitume wake kwa waja wake | Mwenye kuyaendesha Mambo peke yake | Mwenye kuzingira kila kitu kwa kukitambua |
| Mwenye kuhifadhi Mwenye kushahidilia | Msimamizi | Mwenye kutosheleza | Mwenye Wasaa | Wa Haki |
| Mzuri | Mtaratibu | Mwenye Aibu | Mwingi wa kusitiri | Mwenye Uungu |
| Mwenye kuzuia | Mkunjufu | Mtoaji | Mwenye kutanguliza | Mwenye kuchelewesha |
| Mwenye kubainisha | Mtoaji au Mpaji | Msimamizi wa kila kitu | Msimamizi | Mwenye kunusuru |
| Mponyaji | Mwenye kufanya atakacho kwenye ufalme wake -Mfalme wa | Mwenye kuwakusanya watu | Nuru ya Mbinguni na Aridhini | Mwenye Utukufu na Ukarimu |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **Wafalme-** | | | |
| **Aliyezianzisha Mbingu na Ardhi baada ya kutokuwepo kabla.[2]** | | | | |

Kwa Jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu

[2] Tazama majina haya pamoja na dalili zake kutoka kwenye Qur'ani na Sunnah katika kitabu (Sherhu Asmaai llahi Al-husnaa fii dhail-kitaabu wa Sunnah).... cha Mtunzi.

# Utangulizi

Kila sifa njema ni zake Allah, tunamsifu, na tunamtaka msaada, na tunamtaka msamaha, na tunajikinga kwa Allah kutokana na shari za nafsi zetu, na kutokana na ubaya wa matendo yetu, atakaye ongozwa na Allah hakuna wa kumpoteza, na atakaye potezwa hakuna wa kumuongoza,Na nina shuhudia hapana mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa ni Allah peke yake, na nina shuhudia ya kwamba Muhammadi ni mja wake na Mtume wake, rehema na amani ziwe juu yake na Maswahaba wake na watakao wafuata kwa wema mpaka siku ya Kiyama, na kufanya wingi wa kujisalimisha. Baada ya hayo;

Huu ni ufupisho wa kitabu changu (Adhkaaru waduaau wal-ilaaji biruqaa minal-kitabi wasunnati)[3]Nimefanya ufupisho ndani yake kwa kugawanya Dua (maombi), ili iwe wepesi kwa kunufaika kwacho, na nimezidisha juu yake Dua (maombi), na faida zenye manufaa, akipenda Allah Mtukufu,Na nina muomba Allah -Aliyetakasika na

[3] Na kimechapishwa kitabu asili kilicho tajwa, Al-hamdulillah, (kila sifa njema ni zake Allah), pamoja na kuzielezea Hadithi zake kuzielezea kulikowekwa wazi katika juzuu nne: Al-Adhkaaru (Hisnul-Muslim) katika juzuu ya kwanza na ya pili, na Dua katika juzuu ya tatu, na tiba na kisomo cha ruqya katika juzuu ya nne.

kutukuka- kwa majina yake mazuri na sifa zake zilizo juu ajaaliye (kitabu hiki) kiwe ni kwa ajili ya kutafuta radhi zake Mtukufu, hakika yeye ni msimamizi wa hilo na ni mueza juu ya hilo.

Na Allah ampe rehema na amani, na amjaze baraka Nabii wetu Muhammadi, na juu ya watu wake na Maswahaba wake, na walio mfuata kwa wema mpaka siku ya Kiyama.

**Amekiandika (kitabu hiki)**

**Said bin Ally bin Wahf Al-qahtaani**

**Kimehaririwa mwezi Shaban 1408 H**

# Ubora (fadhila) za maombi

Amesema Allah Mtukufu:

[4]"Na amesema Mola wenu niombeni nitakujibuni hakika wale wafanyao kiburi kunako ibada yangu hakika wataingia ndani ya moto wa Jahanamu wakiwa madhalili" (4) Na akasema-Aliye takasika na kutukuka-:

﴿وَإِذَا سَأَلَكَ عِبَادِي عَنِّي فَإِنِّي قَرِيبٌۖ أُجِيبُ دَعْوَةَ ٱلدَّاعِ إِذَا دَعَانِۖ فَلْيَسْتَجِيبُواْ لِي وَلْيُؤْمِنُواْ بِي لَعَلَّهُمْ يَرْشُدُونَ ١٨٦﴾ [البقرة: 186]

"Na waja wangu watakapo kuuliza khabari zangu, basi Mimi nipo karibu. Naitika maombi ya mwombaji anapo niomba. Basi na waniitikie Mimi, na waniamini Mimi, ili wapate kuongoka".[5]

---

[4] Ameitoa hadithi hii Al-Haakimu,154/1, na kwenye kitabu cha Zawaaidu Musnadi Al-Bazaar. 2/442, kwa nambari 2177, na ameitoa Attabaraaniy katika Duaa, kwa nambari 1435, na akasema Al-Haythami katika kitabu Majmau Azawaaidi,10/179:(Isnaadu Atabaraaniy jayidu) Mapokezi ya Tabarani ni mazuri.

[5] Suratul-Baqarah: 186.

Na alisema Mtume rehema na amani za Allah ziwe juu yake: "Dua -maombi- ndio ibada,amesema Mola wenu Mlezi wenu:

((ادْعُونِي أَسْتَجِبْ لَكُمْ))[6]، "Niombeni nitakujibuni"[7] Na amesema Mtume rehema na amani za Allah ziwe juu yake: "Hakika Mola wenu ametakasika na kutukuka ni Mwenye aibu mkarimu anamuonea aibu mja wake atakapo nyanyua mikono yake kumuelekezea (Allah) kisha amrejeshe patupu"[8],na alisema Mtume rehema na amani za Allah ziwe juu yake: "Hakuna muislamu yeyote ataomba maombi hakuna ndani ya maombi hayo madhambi wala kukata udugu, isipokuwa Allah atampa kwa maombi hayo moja kati ya mambo matatu: Moja

---

[6] Abuu Daaud, 2/78, kwa nambari 1481, na Tirmidhiy, 5/211, kwa nambari 2959, na Ibn Majah, 2/1258, kwa nambari 3828, na ameisahihisha Alban katika sahihi Al-Jaamii Asaghiiri, 3/150 na ameisahihisha Ibn Majah, 2/324.

[7] Ameitoa Abuu Daaud, 2/78, kwa nambari 1488 na Tirmidhiy, 5/557, kwa nambari 3556 na Ibn Majah, 2/1272, kwa nambari 3865, na akasema Ibn Hajar: (Sanadi yake ni nzuri), na ameisahihisha Al-Albaani katika Sahihi Attirimidhi 3/179.

[8] Ameitoa Tirmidhi, 5/566. na 5/462, kwa nambari 3573, na Ahmad, 3/18, kwa nambari 11150, na ameisahihisha Albaani katika Sahihi Al-Jaami Assaghiir, 5/116, na sahihi sunani Attrimidhi, 3/140.

amuharakishie maombi yake, au amlimbikizie ili amlipe siku ya Kiyama, au amuondoshee katika mabaya mfano wake" Wakasema: (Maswahaba) kwa hiyo tuzidishe? Akasema: "Allah ni mwenye kuzidisha mara dufu"[9].

Adabu za maombi na sababu za kujibiwa (10)[10]

1- Kutakasa matendo kwa ajili ya Allah.

2- Ataanza kwa kumtukuza Allah na kumsifu, kisha atamtakia rehema Mtume rehema na amani ziwe juu yake na atamalizia kwa kumtakia rehema Mtume.

3- Kutilia manani katika maombi, na kuwa na yakini kwa kujibiwa.

4- Kukithirisha maombi na kutofanya haraka ya kujibiwa.

5- Moyo kuhudhuria katika maombi.

6- Kuomba kipindi cha faraja na dhiki.

7- Asiombwe isipokuwa Allah.

8- Kuto kuomba maombi mabaya dhidi ya mke, mali, mtoto, na nafsi.

---

[9] Tazama asili, 3/863-926

[10] Tazama adabu hizi na sababu za kujibiwa pamoja na dalili zake katika asili, 3-927-975.

9- Kushusha sauti wakati wa maombi iwe baina ya kuishusha na kuidhihirisha.

10- Kukiri makosa, na kutaka msamaha wa kosa, na kuitambua neema, na kumshukuru Allah kwa neema hizo.

11- Kuto kujilazimisha kuomba maombi yaliyo pangika kwa vina.

12- Kujishusha na kunyenyekea, na kuwa na shauku ya kupata mazuri na kuwa na hofu ya adhabu na shari.

13- Kurejesha vitu vilivyo dhulumiwa pamoja na kutubia

14- Kuomba mara tatu tatu.

15- Kuelekea kibla.

16- Kunyanyua mikono wakati wa kuomba.

17- Kushika udhu wakati wa kuomba kama kutakuwa na wepesi.

18- Asichupe mipaka katika maombi.

19- Aanze kujiombea mwenyewe pindi atakapo muombea mtu mwingine[11]

---

[11] Hakika imethibiti kutoka kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake kuwa yeye alianza kujiombea mwenyewe, na imethibiti vile vile kuwa yeye hakuanza kujiombea mwenyewe, kama alivyo muombea Anasi na Ibn Abasi, na Ummu Ismail na wengineo, tazama ufafanuzi katika mambo

20- Apitie kwa Allah kwa majina yake yaliyo mazuri, na kwa sifa zake zilizo za juu, au kwa matendo mazuri aliyo yafanya muombaji yeye mwenyewe, au kwa kuombewe na mtu mwema aliyepo akiwa hai.

21- Kiwe chakula na kinywaji na mavazi vya tokana na pato la halali.

22- Asiombe ubaya au kukata udugu.

23- Aamrishe wema na akataze mabaya.

24- Ajiweke mbali na kila aina na maasi.

Nyakati na hali na sehemu zinazo kubalika ndani yake dua (12)[12]

1- Usiku wa cheo. (unapatikana ndani ya masiku kumi ya mwisho ndani ya mwezi wa Ramadhani)

2- Ndani ya kiza cha usiku wa mwisho karibu na alfajiri (usiku wa manane)

4- Baada ya sala za lazima.

---

haya ndani ya kitabu: Sherhe Annawawiy lisahihi Muslimu. 15/144, Watuhfatul-Ahwadhi sharhe sunani Attirmidhiy, 9/328, Wafat-hul-Baari sharhe sahihi Al-Bukhaar, 1-281.

[12] Tazama nyakati hizi na hali na sehemu pamoja na dalili zake kwa ufafanuzi katika asili. 3/975-1117.

4- Baina na adhana na kusimama kwa sala

5- Nyakati za kila usiku (muda wa kujibiwa)

6- Wakati panapo nadiwa swala za lazima.

7- Mvua inapo nyesha.

8- Wakati jeshi linapo tembea kupigania njia ya Allah.

9- Nyakati inayopatikana siku ya ijumaa.

Na kauli yenye nguvu katika wakati huo ni wakati wa mwisho katika nyakati za Lasiri siku ya ijumaa, na inaweza ikawa ni wakati wa hotuba na swala.

10- Wakati wakunywa maji ya Zamzam pamoja na kuwa na nia ya kweli.

11- Katika sijida.

12- Wakati unapozinduka kutoka kwenye usingizi wa usiku, na kuomba maombi yaliyo thibiti katika wakati huo.

13- Atakapo lala hali ya kujitwaharisha kisha akazinduka usiku na akaomba.

14- Wakati wa kuomba (laa ilaha illa anta sub-haanaka inni kuntu mina dhaalimin).

15- Kuwaombea watu baada ya kifo cha mtu.

16- Kuomba baada ya kumsifia Allah na kumtakia rehema Mtume rehema na amani ziwe juu yake katika kikao cha mwisho.

17- Wakati wa kumuomba Allah kwa jina lake tukufu ambalo akiombwa hujibu, na akihitajiwa hutoa kwa kupitia jina hilo (13).[13]

18- Muislamu kumuombea ndugu yake muislamu bila ya yeye kuwepo.

19- Maombi ya siku ya Arafa katika viwanja vya Arafa.

20- Maombi ndani ya mwezi wa Ramadhani.

21- Maombi pindi wanapo jikusanya waislamu katika vikao vya kumtaja Allah.

22- Wakati wa kuomba pindi mtu anapo patwa na matatizo kwa kusema (Inna lillaahi wa innaa ilaihi raajiuuni, Allaahumma ajurnii fii muswiibatii, wa akh-lif lii khairan minha).

23- Kuomba wakati moyo unapokuwa umemuelekea Allah, na wakati inapozidi ikhilaswi (kufanya matendo kwa ajili ya Allah).

---

[13] Tazama jina la Allah tukufu kwenye hadithi nambari 203, na nambari 104, na nambari 105 kutoka kwenye kitabu hiki.

24- Maombi ya aliye dhulumiwa kwa aliye mdhulumu.

25- Maombi kwa mzazi kumuombea mtoto wake, na mzazi kumuombea mabaya mtoto wake.

26- Maombi ya msafiri.

27- Maombi ya mfungaji mpaka atakapo fungua.

28- Maombi ya mfungaji wakati anapo fungua.

29- Moambi ya mtu mwenye matatizo.

30- Maombi ya imamu muadilifu.

31- Maombi ya mtoto mwema kwa wazazi wake.

32- Maombi baada ya kutawadha pindi anapo omba dua iliyothibiti katika hilo.

33- Maombi baada ya kutupa mawe kwenye kiguzo kidogo (kwa walio kwenda Hija)

34- Maombi baada ya kutupa mawe kwenye kiguzo cha kati (kwa waliokwenda Hija)

35- Maombi wakati unapokuwa ndani ya Al-kaba, na atakaye swali ndani ya uzio wa Ismail (unao ambatana na Al-kaaba) ambao ni sehemu ya Al-kaba.

36- Maombi unapokuwa juu ya Swafa (kwa wafanyao ibada ya Hija au Umra)

37- Maombi anapokuwa juu ya Marwa (kwa wanaofanya ibada ya Hija au Umra)

38- Maombi unapokuwa Muzdalifa (sehemu inayofuata baada ya kutoka Arafa)

Na muumini anamuomba Mola wake popote atakapo kuwepo kwa kudumu na hali hiyo, amesema Allah aliyetakasika na kutukuka:

﴿وَإِذَا سَأَلَكَ عِبَادِى عَنِّى فَإِنِّى قَرِيبٌ أُجِيبُ دَعْوَةَ ٱلدَّاعِ إِذَا دَعَانِ فَلْيَسْتَجِيبُوا۟ لِى وَلْيُؤْمِنُوا۟ بِى لَعَلَّهُمْ يَرْشُدُونَ ١٨٦﴾ [البقرة: 186]

"Na waja wangu watakapo kuuliza kuhusu mimi, Mimi nipo karibu. Naitika maombi ya muombaji anapo niomba. Basi na waniitikie Mimi, na waniamini Mimi, ili wapate kuongoka".14 Lakini nyakati hizi, na hali, na sehemu zinakuwa ni mahususi kwa kuzidisha mazingatio.

---

[14] Suratul-Baqarah: 186

# Maombi kupitia Qur'ani na Sunna

Kila sifa njema ni zake Allah peke yake, na rehema na amani ziwe kwa ambaye hakuna nabii baada yake.

﴿بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ ١ ٱلۡحَمۡدُ لِلَّهِ رَبِّ ٱلۡعَٰلَمِينَ ٢ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ ٣ مَٰلِكِ يَوۡمِ ٱلدِّينِ ٤ إِيَّاكَ نَعۡبُدُ وَإِيَّاكَ نَسۡتَعِينُ ٥ ٱهۡدِنَا ٱلصِّرَٰطَ ٱلۡمُسۡتَقِيمَ ٦ صِرَٰطَ ٱلَّذِينَ أَنۡعَمۡتَ عَلَيۡهِمۡ غَيۡرِ ٱلۡمَغۡضُوبِ عَلَيۡهِمۡ وَلَا ٱلضَّآلِّينَ ٧﴾ [الفاتحة: 1-7]

1-"Kwa Jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu* Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote * Mwingi wa rehema mwenye kurehemu * Mfalme wa siku ya mwisho* Ni wewe peke yako tunaye kuabudu na ni wewe peke yako tunaye kutaka msaada* Tuongoze njia iliyo nyooka* Njia ya wale ulio waneemesha juu yao, si ya wale ulio wakasirikia wala walio potea" [15].

﴿...رَبَّنَا تَقَبَّلۡ مِنَّآۖ إِنَّكَ أَنتَ ٱلسَّمِيعُ ٱلۡعَلِيمُ ١٢٧﴾ [البقرة: 127]

---

[15] Suratul-Faatiha: 1-7.

2- "Mola wetu tukubalie nasi hakika wewe ni mwenye kusikia mjuzi" [16].

﴿رَبَّنَا وَٱجۡعَلۡنَا مُسۡلِمَيۡنِ لَكَ وَمِن ذُرِّيَّتِنَآ أُمَّةٗ مُّسۡلِمَةٗ لَّكَ وَأَرِنَا مَنَاسِكَنَا وَتُبۡ عَلَيۡنَآۖ إِنَّكَ أَنتَ ٱلتَّوَّابُ ٱلرَّحِيمُ ١٢٨﴾ [البقرة: 128]

3- "Na tusamehe makosa yaliyo juu yetu hakika wewe ni mwenye kukubali msamaha mrehemevu"[17].

﴿... رَبَّنَآ ءَاتِنَا فِي ٱلدُّنۡيَا حَسَنَةٗ وَفِي ٱلۡأٓخِرَةِ حَسَنَةٗ وَقِنَا عَذَابَ ٱلنَّارِ ٢٠١﴾ [البقرة: 201]

4- "Mola wetu Mlezi, tupe duniani mema na akhera tupe mema na utukinge na adhabu ya moto" [18].

﴿... سَمِعۡنَا وَأَطَعۡنَاۖ غُفۡرَانَكَ رَبَّنَا وَإِلَيۡكَ ٱلۡمَصِيرُ ٢٨٥﴾ [البقرة: 285]

5-"Tumesikia na tumetii msamaha ni wa kwako Mola wetu Mlezi, na kwako ndio marejeo" [19].

---

[16] Suratul-Baqara: 127.

[17] Suratul-Baqara: 128.

[18] Suratul-Baqara: 201.

[19] Suratul-Baqara: 285.

﴿... رَبَّنَا لَا تُؤَاخِذۡنَآ إِن نَّسِينَآ أَوۡ أَخۡطَأۡنَاۚ رَبَّنَا وَلَا تَحۡمِلۡ عَلَيۡنَآ إِصۡرٗا كَمَا حَمَلۡتَهُۥ عَلَى ٱلَّذِينَ مِن قَبۡلِنَاۚ رَبَّنَا وَلَا تُحَمِّلۡنَا مَا لَا طَاقَةَ لَنَا بِهِۦۖ وَٱعۡفُ عَنَّا وَٱغۡفِرۡ لَنَا وَٱرۡحَمۡنَآۚ أَنتَ مَوۡلَىٰنَا فَٱنصُرۡنَا عَلَى ٱلۡقَوۡمِ ٱلۡكَٰفِرِينَ ٢٨٦﴾ [البقرة: 286]

6- "Mola wetu Mlezi, usitupatilize tutakapo sahau au tutakapo kosea, Mola wetu, wala usitubebeshe juu yetu mizigo (ya madhambi) kama ulivyo wabebesha wale waliokuwa kabla yetu, mola wetu, wala usitubebeshe yale tusiyo yaweza kuyabeba na utusamehe na utufutie madhambi na utuhurumie wewe ndiye msimamizi wetu basi tunusuru juu ya watu wapingaji" [20].

﴿رَبَّنَا لَا تُزِغۡ قُلُوبَنَا بَعۡدَ إِذۡ هَدَيۡتَنَا وَهَبۡ لَنَا مِن لَّدُنكَ رَحۡمَةًۚ إِنَّكَ أَنتَ ٱلۡوَهَّابُ ٨﴾ [آل عمران: 8]

7- "Mola wetu Mlezi, usizipotoe nyoyo zetu baada ya kwisha tuongoa, na utupe kutoka kwako rehema hakika wewe ndiye Mpaji" [21].

---

[20] Suratul-Baqarah: 286.

[21] Suratul-Al-Imraan: 8.

﴿... رَبَّنَآ إِنَّنَآ ءَامَنَّا فَٱغۡفِرۡ لَنَا ذُنُوبَنَا وَقِنَا عَذَابَ ٱلنَّارِ١٦﴾ [آل عمران: 16]

8- "Mola wetu Mlezi! Hakika sisi tumeamini basi tufutie madhambi yetu na utukinge na adhabu ya moto")[22].

﴿... رَبِّ هَبۡ لِي مِن لَّدُنكَ ذُرِّيَّةٗ طَيِّبَةًۖ إِنَّكَ سَمِيعُ ٱلدُّعَآءِ٣٨﴾ [آل عمران: 38]

9- "Mola wangu Mlezi! Nipe kutoka kwako kizazi chema hakika wewe ni mwenye kusikia maombi yangu" [23].

﴿رَبَّنَآ ءَامَنَّا بِمَآ أَنزَلۡتَ وَٱتَّبَعۡنَا ٱلرَّسُولَ فَٱكۡتُبۡنَا مَعَ ٱلشَّٰهِدِينَ٥٣﴾ [آل عمران: 53]

10- "Mola wetu Mlezi! Tumeamini yale uliyo yateremsha na tukamfuata Mtume, basi tuandike pamoja na mashahidi" [24].

---

[22] Suratul-Al-Imraan: 16.

[23] Suratul-Al-Imraan: 38.

[24] Suratul-Al-Imraan: 53

﴿وَمَا كَانَ قَوۡلَهُمۡ إِلَّآ أَن قَالُواْ رَبَّنَا ٱغۡفِرۡ لَنَا ذُنُوبَنَا وَإِسۡرَافَنَا فِيٓ أَمۡرِنَا وَثَبِّتۡ أَقۡدَامَنَا وَٱنصُرۡنَا عَلَى ٱلۡقَوۡمِ ٱلۡكَٰفِرِينَ١٤٧﴾ [آل عمران: 147]

11- "Mola wetu Mlezi! Tusamehe madhambi yetu na kupita kwetu kiasi katika mambo yetu, na isimamishe imara miguu yetu na utunusuru tuwashinde kaumu ya makafiri" [25].

﴿... رَبَّنَا مَا خَلَقۡتَ هَٰذَا بَٰطِلٗا سُبۡحَٰنَكَ فَقِنَا عَذَابَ ٱلنَّارِ ١٩١ رَبَّنَآ إِنَّكَ مَن تُدۡخِلِ ٱلنَّارَ فَقَدۡ أَخۡزَيۡتَهُۥۖ وَمَا لِلظَّٰلِمِينَ مِنۡ أَنصَارٖ١٩٢ رَّبَّنَآ إِنَّنَا سَمِعۡنَا مُنَادِيٗا يُنَادِي لِلۡإِيمَٰنِ أَنۡ ءَامِنُواْ بِرَبِّكُمۡ فَـَٔامَنَّاۚ رَبَّنَا فَٱغۡفِرۡ لَنَا ذُنُوبَنَا وَكَفِّرۡ عَنَّا سَيِّـَٔاتِنَا وَتَوَفَّنَا مَعَ ٱلۡأَبۡرَارِ١٩٣ رَبَّنَا وَءَاتِنَا مَا وَعَدتَّنَا عَلَىٰ رُسُلِكَ وَلَا تُخۡزِنَا يَوۡمَ ٱلۡقِيَٰمَةِۖ إِنَّكَ لَا تُخۡلِفُ ٱلۡمِيعَادَ ١٩٤﴾ [آل عمران: 191-194]

12-"Mola wetu Mlezi! Hukuviumba hivi bure, utakasifu ni wako basi tukinge na adhabu ya moto* Mola wetu Mlezi! Hakika unaye mtia motoni umemdhalilisha na hawana watu waovu wakuwanusuru* Mola wetu Mlezi hakika sisi tumemsikia mwenye kuita akiita katika imani

[25] Suratul-Al-Imraan: 147.

kwamba, muaminini Mola wenu Mlezi, nasi tukaamini, basi tusamehe madhambi yetu na utufutie makosa yetu na utufishe pamoja na watu wema* Mola wetu Mlezi na utupe uliyo tuahidi kwa Mitume wako na wala usitudhalilishe siku ya Kiyama hakika wewe huvunji ahadi"[26].

﴿... رَبَّنَآ ءَامَنَّا فَٱكۡتُبۡنَا مَعَ ٱلشَّٰهِدِينَ ٨٣﴾ [المائدة: 83]

13- "Mola wetu Mlezi! Tumeamini basi tuandike kuwa miongoni mwa mashahidi" [27].

﴿... رَبَّنَا ظَلَمۡنَآ أَنفُسَنَا وَإِن لَّمۡ تَغۡفِرۡ لَنَا وَتَرۡحَمۡنَا لَنَكُونَنَّ مِنَ ٱلۡخَٰسِرِينَ ٢٣﴾ [الأعراف: 23]

4- "Mola wetu Mlezi! Hakika sisi tumedhulumu nafsi zetu na kama huta tusamehe na kutuonea huruma hakika tutakuwa miongoni mwa watu walio pata hasara" [28].

---

[26] Suratul-Al-Imraan: 191-194.

[27] Suratul- Al-Maaidah: 83

[28] Suratul-Al-Araaf: 23.

﴿...رَبَّنَا لَا تَجۡعَلۡنَا مَعَ ٱلۡقَوۡمِ ٱلظَّٰلِمِينَ ﴿٤٧﴾﴾ [الأعراف: 47]

15- "Mola wetu Mlezi! Usitujaalie kuwa miongoni mwa watu madhalimu" [29].

﴿... أَنتَ وَلِيُّنَا فَٱغۡفِرۡ لَنَا وَٱرۡحَمۡنَاۖ وَأَنتَ خَيۡرُ ٱلۡغَٰفِرِينَ ﴿١٥٥﴾ ۞ وَٱكۡتُبۡ لَنَا فِي هَٰذِهِ ٱلدُّنۡيَا حَسَنَةٗ وَفِي ٱلۡأٓخِرَةِ ... ﴿١٥٦﴾﴾ [الأعراف: 155-156]

16- Ewe Mwenyezi Mungu! "Wewe ndiye msimamizi wetu basi tusamehe sisi na utuhurumie, hakika Wewe ni mbora wa kusamehe* Na utuandikie sisi katika hii dunia mema na siku ya mwisho (vile vile utulipe mema)))[30].

﴿... حَسۡبِيَ ٱللَّهُ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا هُوَۖ عَلَيۡهِ تَوَكَّلۡتُۖ وَهُوَ رَبُّ ٱلۡعَرۡشِ ٱلۡعَظِيمِ ﴿١٢٩﴾﴾ [التوبة: 129]

17- "Ananitosha Allah hapana mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Yeye naye ni Mola Mlezi wa Arshi tukufu".[31].

---

29 - Suratul-Al-Araaf: 47

30 Surataul-Al-Araaf: 155-156.

31 Suratul-Taubah: 129.

﴿... رَبَّنَا لَا تَجۡعَلۡنَا فِتۡنَةٗ لِّلۡقَوۡمِ ٱلظَّٰلِمِينَ ٨٥ وَنَجِّنَا بِرَحۡمَتِكَ مِنَ ٱلۡقَوۡمِ ٱلۡكَٰفِرِينَ ٨٦﴾ [يونس: 85-86]

18-"Mola wetu Mlezi! Usitufitinishe kwa watu madhalimu* Na utukinge kwa Rehema zako dhidi ya watu makafiri"[32].

﴿... رَبِّ إِنِّيٓ أَعُوذُ بِكَ أَنۡ أَسۡـَٔلَكَ مَا لَيۡسَ لِي بِهِۦ عِلۡمٞۖ وَإِلَّا تَغۡفِرۡ لِي وَتَرۡحَمۡنِيٓ أَكُن مِّنَ ٱلۡخَٰسِرِينَ ٤٧﴾ [هود: 47]

19- "Mola wangu Mlezi! Hakika mimi najikinga kwako kuto kukuomba mambo nisiyo kuwa na ujuzi nayo na kama huta nisamehe na kunihurumia nitakuwa miongoni mwa watu walio pata hasara" [33].

﴿...ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلۡأَرۡضِ أَنتَ وَلِيِّۦ فِي ٱلدُّنۡيَا وَٱلۡأٓخِرَةِۖ تَوَفَّنِي مُسۡلِمٗا وَأَلۡحِقۡنِي بِٱلصَّٰلِحِينَ ١٠١﴾ [يوسف: 101]

20- Ewe Mwenyezi Mungu "Ewe Muumba wa mbingu na ardhi wewe ndiyo Mlezi wangu duniani na

---

[32] Suratu-Yuunus: 85-86

[33] Suratu-Huud: 47

akhera nifishe nikiwa ni muislamu na unikutanishe na waja wema"[34]

﴿ رَبِّ ٱجۡعَلۡ هَٰذَا ٱلۡبَلَدَ ءَامِنٗا وَٱجۡنُبۡنِي وَبَنِيَّ أَن نَّعۡبُدَ ٱلۡأَصۡنَامَ﴿٣٥﴾﴾ [إبراهيم: 35]

21- "Mola wangu Mlezi! Ujaalie mji huu ni wenye amani na uniepushe mimi na kizazi changu tusiabudu masanamu" [35].

﴿رَبِّ ٱجۡعَلۡنِي مُقِيمَ ٱلصَّلَوٰةِ وَمِن ذُرِّيَّتِيۚ رَبَّنَا وَتَقَبَّلۡ دُعَآءِ﴿٤٠﴾﴾ [إبراهيم: 40]

22- "Mola wangu Mlezi! Nijaalie niwe ni mwenye kusimamisha swala, na katika kizazi changu pia. Ewe Mola wetu Mlezi, na ipokee dua yangu"[36].

﴿رَبَّنَا ٱغۡفِرۡ لِي وَلِوَٰلِدَيَّ وَلِلۡمُؤۡمِنِينَ يَوۡمَ يَقُومُ ٱلۡحِسَابُ﴿٤١﴾﴾ [إبراهيم: 41]

23- "Mola wetu Mlezi nisamehe mimi na wazazi wangu na waumini siku itakapo simama hesabu".

﴿... رَبَّنَآ ءَاتِنَا مِن لَّدُنكَ رَحۡمَةٗ وَهَيِّئۡ لَنَا مِنۡ أَمۡرِنَا رَشَدٗا﴿١٠﴾﴾ [الكهف: 10]

---

[34] - Surat-Yunus: 101: Angalia kwa ajili ya faida: Kitabu Al-Fawaaidi cha Ibn Qayyimi, Ukurasa wa 436-437.

[35] Suratu: Ibrahimu: 35

[36] Surat Ibrahim: 41].

24- "Mola wetu Mlezi! Tupe kutoka kwako huruma, na ututengenezee uongofu katika jambo letu"[37].

﴿قَالَ رَبِّ ٱشْرَحْ لِي صَدْرِي ۝٢٥ وَيَسِّرْ لِيٓ أَمْرِي ۝٢٦ وَٱحْلُلْ عُقْدَةً مِّن لِّسَانِي ۝٢٧ يَفْقَهُوا۟ قَوْلِي ۝٢٨﴾ [طه: 25-28]

25- "Mola wangu Mlezi kikunjue kifua changu* Na ulifanyie wepesi jambo langu Na uniondoshee uzito kwenye ulimi wangu ili waweze kulifahamu maneno yangu"[38].

﴿... رَّبِّ زِدْنِي عِلْمًا ۝١١٤﴾ [طه: 114]

26- "Mola wangu Mlezi! Nizidishie elimu" [39].

﴿.... لَّآ إِلَٰهَ إِلَّآ أَنتَ سُبْحَٰنَكَ إِنِّي كُنتُ مِنَ ٱلظَّٰلِمِينَ ۝٨٧﴾ [الأنبياء: 87]

27- "Hapana mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa wewe, utakasifu ni wako, hakika mimi nilikuwa miongoni mwa watu madhalimu"[40].

---

[37] Suratul-Kahf: 10].

[38] Suratu Twaha: 25-28].

[39] Suratu Twaha: 114].

[40] Suratul-Anbiyaa: 87].

﴿وَزَكَرِيَّآ إِذۡ نَادَىٰ رَبَّهُۥ رَبِّ لَا تَذَرۡنِي فَرۡدٗا وَأَنتَ خَيۡرُ ٱلۡوَٰرِثِينَ ٨٩﴾ [الأنبياء: 89]

28- "Mola wangu Mlezi! Usiniache mpweke na wewe ndiye mbora wa wanao rithi" [41].

﴿وَقُل رَّبِّ أَعُوذُ بِكَ مِنۡ هَمَزَٰتِ ٱلشَّيَٰطِينِ ٩٧ وَأَعُوذُ بِكَ رَبِّ أَن يَحۡضُرُونِ ٩٨﴾ [المؤمنون: 97-98]

29- "Mola wangu Mlezi! Najikinga kwako kutokana na wasi wasi wa mashetani* Na ninajikinga kwako Mola wangu Mlezi wasinikaribie"[42].

﴿... رَبَّنَآ ءَامَنَّا فَٱغۡفِرۡ لَنَا وَٱرۡحَمۡنَا وَأَنتَ خَيۡرُ ٱلرَّٰحِمِينَ ١٠٩﴾ [المؤمنون: 109]

30- "Mola wetu Mlezi! Tumeamini; basi tusamehe na utuhurumie, nawe ndiye mbora wa wenye kuhurumia" [43].

﴿... رَبَّنَا ٱصۡرِفۡ عَنَّا عَذَابَ جَهَنَّمَۖ إِنَّ عَذَابَهَا كَانَ غَرَامًا ٦٥﴾ [الفرقان: 65]

---

[41] Suratul-Anbiyaa: 89].

[42] Suratul-Muuminuna: 97-98].

[43] Suratu-Al-Muuminuna: 109]

31- "Mola wangu Mlezi! Samehe na urehemu nawe ni mbora wa wenye kurehemu"[44].

﴿وَٱلَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَا ٱصۡرِفۡ عَنَّا عَذَابَ جَهَنَّمَۖ إِنَّ عَذَابَهَا كَانَ غَرَامًا ٦٥ إِنَّهَا سَآءَتۡ مُسۡتَقَرّٗا وَمُقَامٗا ٦٦﴾ [الفرقان: 65-66]

32- "Mola wetu Mlezi! Tuondoshee juu yetu adhabu ya Moto wa Jahannam hakika adhabu yake ikimpata mtu haimwachi* Hakika adhabu yake ni yenye makazi na mafikio mabaya" [45].

﴿... رَبَّنَا هَبۡ لَنَا مِنۡ أَزۡوَٰجِنَا وَذُرِّيَّٰتِنَا قُرَّةَ أَعۡيُنٖ وَٱجۡعَلۡنَا لِلۡمُتَّقِينَ إِمَامًا ٧٤﴾ [الفرقان: 74]

33- "Mola wetu Mlezi! Tupe sisi kutoka kwa wake zetu na vizazi vyetu vitulizo vya macho na utufanye viongozi kwa wamchao Allah"[46].

﴿رَبِّ هَبۡ لِي حُكۡمٗا وَأَلۡحِقۡنِي بِٱلصَّٰلِحِينَ ٨٣ وَٱجۡعَل لِّي لِسَانَ صِدۡقٖ فِي ٱلۡأٓخِرِينَ ٨٤ وَٱجۡعَلۡنِي مِن وَرَثَةِ جَنَّةِ ٱلنَّعِيمِ ٨٥﴾ [الشعراء: 83-85]

---

[44] Suratu-Al-muuminuna: 118].

[45] Surat-Al-Furqaan: 65-66].

[46] Surat-Al-Furqaan: 84]

34- "Mola wangu Mlezi! Nipe mimi hekima na unikutanishe na waja wema* Na unijalie nitajwe kwa wema kwa watu wakaokuja baadaye* Na unijalie ni mwenye kurithi Bustani za neema" [47].

﴿وَلَا تُخۡزِنِي يَوۡمَ يُبۡعَثُونَ٨٧ يَوۡمَ لَا يَنفَعُ مَالٞ وَلَا بَنُونَ٨٨ إِلَّا مَنۡ أَتَى ٱللَّهَ بِقَلۡبٖ سَلِيمٖ٨٩﴾ [الشعراء: 87-89]

35- "Na wala usinihuzunishe siku watakayo fufuliwa watu* Siku ambayo mali wala watoto havitomfaa mtu* Isipokuwa yule atakaye muendea Allah kwa moyo ulio salimika . [48]"

﴿... رَبِّ أَوۡزِعۡنِيٓ أَنۡ أَشۡكُرَ نِعۡمَتَكَ ٱلَّتِيٓ أَنۡعَمۡتَ عَلَيَّ وَعَلَىٰ وَٰلِدَيَّ وَأَنۡ أَعۡمَلَ صَٰلِحٗا تَرۡضَىٰهُ وَأَدۡخِلۡنِي بِرَحۡمَتِكَ فِي عِبَادِكَ ٱلصَّٰلِحِينَ ١٩﴾ [النمل: 19]

36- "Mola wangu Mlezi! Niwezeshe kuwa ni mwenye kushukuru neema zako ambazo ulizo nineemesha juu yangu na juu ya wazazi wangu na

---

[47] Surat-Ashuaraa: 83-85]

[48] Surat-Ashuaraa: 87-89].

nifanye matendo mazuri utakayo yaridhia na uniingize kwa huruma yako katika waja wako wema" [49].

﴿قَالَ رَبِّ إِنِّي ظَلَمْتُ نَفْسِي فَٱغْفِرْ لِي فَغَفَرَ لَهُۥٓۚ إِنَّهُۥ هُوَ ٱلْغَفُورُ ٱلرَّحِيمُ ١٦﴾ [القصص: 16]

37- "Mola wangu Mlezi! Hakika mimi nimeidhulimu nafsi yangu basi nisamehe" [50].

﴿... رَبِّ نَجِّنِي مِنَ ٱلْقَوْمِ ٱلظَّٰلِمِينَ ٢١﴾ [القصص: 21]

38- "Mola wangu Mlezi! Niokoe kutokana na watu madhalimu"[51].

﴿... عَسَىٰ رَبِّيٓ أَن يَهْدِيَنِي سَوَآءَ ٱلسَّبِيلِ ٢٢﴾ [القصص: 22]

39- "Hakika Mola wangu Mlezi ataniongoza katika njia iliyo ya sawa" [52].

﴿... رَبِّ إِنِّي لِمَآ أَنزَلْتَ إِلَيَّ مِنْ خَيْرٍ فَقِيرٌ ٢٤﴾ [القصص: 24]

---

[49] Surat-Al-Nnaml: 19].

[50] Surat-Al-Qasas: 16].

[51] Surat-Al-Qasas: 21].

[52] Surat-Al-Qasas: 22].

40- "Mola wangu Mlezi! Hakika mimi ni mhitaji wa kheri utakayo niteremshia"[53].

﴿قَالَ رَبِّ ٱنصُرۡنِي عَلَى ٱلۡقَوۡمِ ٱلۡمُفۡسِدِينَ ٣٠﴾ [العنكبوت: 30]

41 -"Mola wangu Mlezi! Ninusuru na watu mafisadi hawa"[54].

﴿رَبِّ هَبۡ لِي مِنَ ٱلصَّٰلِحِينَ ١٠٠﴾ [الصافات: 100]

42- "Mola wangu Mlezi! Nitunuku aliye miongoni mwa watenda mema"[55].

﴿...رَبِّ أَوۡزِعۡنِيٓ أَنۡ أَشۡكُرَ نِعۡمَتَكَ ٱلَّتِيٓ أَنۡعَمۡتَ عَلَيَّ وَعَلَىٰ وَٰلِدَيَّ وَأَنۡ أَعۡمَلَ صَٰلِحٗا تَرۡضَىٰهُ وَأَصۡلِحۡ لِي فِي ذُرِّيَّتِيٓۖ إِنِّي تُبۡتُ إِلَيۡكَ وَإِنِّي مِنَ ٱلۡمُسۡلِمِينَ ١٥﴾ [الأحقاف: 15]

43- "Mola wangu Mlezi! Niwezeshe kuwa ni mwenye kushukuru neema zako ulizo nineemesha juu yangu na juu ya wazazi wangu na nifanye matendo

---

[53] Surat-Al-Qasas: 24].

[54] Suarat-Al-Anqabuut: 30].

[55] Surat-Al-Aswaafaat: 100].

mema utakayo ridhia na nitengenezee katika vizazi vyangu hakika mimi nimetubia kwako na hakika mimi ni miongoni mwa waislamu" [56].

﴿... رَبَّنَا ٱغۡفِرۡ لَنَا وَلِإِخۡوَٰنِنَا ٱلَّذِينَ سَبَقُونَا بِٱلۡإِيمَٰنِ وَلَا تَجۡعَلۡ فِي قُلُوبِنَا غِلّٗا لِّلَّذِينَ ءَامَنُواْ رَبَّنَآ إِنَّكَ رَءُوفٞ رَّحِيمٌ ١٠﴾ [الحشر: 10]

44- "Mola wetu Mlezi! Tusamehe sisi na ndugu zetu walio tutangulia kwa imani, na usitujalie ndani ya mioyo yetu chuki kwa wale walio amini, Mola wetu Mlezi! Hakika wewe ni Mpole Mrehemevu"[57].

﴿... رَّبَّنَا عَلَيۡكَ تَوَكَّلۡنَا وَإِلَيۡكَ أَنَبۡنَا وَإِلَيۡكَ ٱلۡمَصِيرُ ٤﴾ [الممتحنة: 4]

45- "Mola wetu Mlezi! juu yako tumetegemea na kwako tunajikurubisha na kwako ndio marejio" [58].

﴿رَبَّنَا لَا تَجۡعَلۡنَا فِتۡنَةٗ لِّلَّذِينَ كَفَرُواْ وَٱغۡفِرۡ لَنَا رَبَّنَآۖ إِنَّكَ أَنتَ ٱلۡعَزِيزُ ٱلۡحَكِيمُ ٥﴾ [الممتحنة: 5]

---

[56] Surat-Al-Ahkaaf: 15].

[57] Surat-Al-Hashr: 10]

[58] Suarat-Al-Mumtahinah: 4].

46- "Mola wetu Mlezi! Usitufanyie mtihani kwa wale walio kufuru. Na utusamehe Mola wetu Mlezi. Hakika wewe ni mwenye nguvu mwenye hekima"[59].

﴿... رَبَّنَآ أَتۡمِمۡ لَنَا نُورَنَا وَٱغۡفِرۡ لَنَآۖ إِنَّكَ عَلَىٰ كُلِّ شَيۡءٖ قَدِيرٞ ٨﴾ [التحريم: 8]

47- "Mola wetu Mlezi! Tukamilishie nuru yetu na utusamehe hakika wewe juu ya kila kitu ni muweza"[60].

﴿رَّبِّ ٱغۡفِرۡ لِي وَلِوَٰلِدَيَّ وَلِمَن دَخَلَ بَيۡتِيَ مُؤۡمِنٗا وَلِلۡمُؤۡمِنِينَ وَٱلۡمُؤۡمِنَٰتِۖ وَلَا تَزِدِ
ٱلظَّٰلِمِينَ إِلَّا تَبَارَۢا ٢٨﴾ [نوح: 28]

48- "Mola wangu Mlezi! Nisamehe mimi na wazazi wangu na aliye ingia nyumbani kwangu hali ya kuwa ni muumini, na kwa waumini wa kiume na waumini wa kike" [61].

﴿...فَهَدَى ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ لِمَا ٱخۡتَلَفُواْ فِيهِ مِنَ ٱلۡحَقِّ بِإِذۡنِهِۦۗ وَٱللَّهُ يَهۡدِي مَن
يَشَآءُ إِلَىٰ صِرَٰطٖ مُّسۡتَقِيمٍ ٢١٣﴾ [البقرة: 213]

---

[59] Surat-Al-Mumtahinah: 5].

[60] Suarat-Al-Tahariim: 8].

[61] Surat-Nuuh: 28].

49- "Ewe Mwenyezi Mungu! Niongoze mimi kwa yale ambayo watu hutofautiana kwayo katika haki kwa idhini yako, hakika wewe humuongoa umtakaye katika njia iliyo nyooka"[62]

﴿يُؤْتِي ٱلْحِكْمَةَ مَن يَشَآءُ ۚ وَمَن يُؤْتَ ٱلْحِكْمَةَ فَقَدْ أُوتِيَ خَيْرًا كَثِيرًا ۗ وَمَا يَذَّكَّرُ إِلَّآ أُوْلُوا۟ ٱلْأَلْبَٰبِ ﴿٢٦٩﴾﴾ [البقرة: 269]

50- "Ewe Mwenyezi Mungu! Nipe hekima ambazo mwenye pewa hekima hizo hakika atakuwa amepewa heri zilizo nyingi"[63]

﴿يُثَبِّتُ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ بِٱلْقَوْلِ ٱلثَّابِتِ فِي ٱلْحَيَوٰةِ ٱلدُّنْيَا وَفِي ٱلْءَاخِرَةِ ۖ ...﴿٢٧﴾﴾ [إبراهيم: 27]

51- "Ewe Mwenyezi Mungu nimakinishe mimi kwa kauli iliyo thabiti katika maisha ya duniani na maisha ya Akhera"[64]

---

[62] Imetoholewa kutoka ndani ya Surat-Al-Baqarah: 213.

[63] Imetoholewa kutoka ndani ya Suarat-Al-Baqarah: 269.

[64] Imetoholewa kutoka ndani ya Surat-Ibrahim: 27.

﴿... ٱللَّهَ حَبَّبَ إِلَيۡكُمُ ٱلۡإِيمَٰنَ وَزَيَّنَهُۥ فِي قُلُوبِكُمۡ وَكَرَّهَ إِلَيۡكُمُ ٱلۡكُفۡرَ وَٱلۡفُسُوقَ وَٱلۡعِصۡيَانَۚ أُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلرَّٰشِدُونَ ٧﴾ [الحجرات: 7]

52- "Ewe Allah tupendezee kwetu sisi imani na uipambe ndani ya nyoyo zetu, na utufanye tuuchukie ukafiri na uovu na upotovu na uasi, Na utujalie kuwa miongoni mwa walio ongoka".[65]

﴿فَٱتَّقُواْ ٱللَّهَ مَا ٱسۡتَطَعۡتُمۡ وَٱسۡمَعُواْ وَأَطِيعُواْ وَأَنفِقُواْ خَيۡرٗا لِّأَنفُسِكُمۡۗ وَمَن يُوقَ شُحَّ نَفۡسِهِۦ فَأُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلۡمُفۡلِحُونَ ١٦﴾ [التغابن: 16]

53- "Ewe Mwenyezi Mungu! Nikinge na tamaa ya nafsi yangu, na unijalie kuwa miongoni mwa walio faulu"[66]

54-"Ewe Mwenyezi Mungu! Tupe hapa katika Dunia (mambo) mazuri, na Akhera utupe mazuri na utukinge na adhabu ya moto"[67]

---

[65] Imetoholewa kutoka ndani ya Suarat-Al-Hujraat: 7.

[66] Imetoholewa kutoka ndani ya Surat-Al-Taghaabun: 16.

[67] Bukhari, kwa nambari: 4522, na nambari 6389, na Muslim, kwa nambari: 2690.

55-Ewe Allah hakika mimi najikinga kwako kutokana na fitina ya moto na adhabu ya moto, na kutokana na fitina ya kaburi na adhabu ya kaburi, na kutokana na shari za fitina za utajiri, na shari za fitina za umasikini, Ewe Allah hakika mimi najikinga kwako kutokana na shari za Masihi Dajali, Ewe Allah usafishe moyo wangu kwa maji ya theluji na baridi, na utakase moyo wangu kutokana na makosa kama jinsi ulivyoitakasa nguo nyeupe kutokana na uchafu, na uniweke mbali baina yangu na baina ya makosa yangu kama ulivyo weka mbali baina ya Mashariki na Magharibi, Ewe Allah hakika mimi najikinga kwako kutokana na uvivu na madhambi na vitu vitakavyo nigharimu (madeni)[68]

56-Ewe Allah hakika mimi najikinga kwako kutokana na kushindwa, na uvivu, na kuogopa, na ukongwe, na ubakhili, na ninajikinga kwako kutokana na adhabu ya kaburi, na kutokana na fitina za uhai na kifo.[69]

57-"Ewe Allah hakika mimi najikinga kwako kutokana na kupatwa na mitihani, na kupatwa na ususuwavu, na

---

[68] Bukhar, nambari 832. Na Muslim nambari 589.

[69] Bukhari nambari 2823, Muslim nambari 2706.

kupatwa na makadirio yenye kuhuzunisha, na kufanya jambo litakalo pelekea kutukanwa na maadui"[70]

58-"Ewe Mwenyezi Mungu nitengenezee dini yangu ambayo ndiyo kinga ya jambo langu, na unitengenezee dunia yangu ambayo kunapatikana maisha yangu, na unitengenezee Akhera yangu ambako kunapatikana kuishi kwangu milele, na unijalie ziada ya uhai kwenye kila lenye heri, na ujalie kifo ni kitulizo changu kutokana na kila shari"[71]

59-"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi nakuomba uongofu, na uchamungu, na kujizuilia na machafu, na kutosheka"[72]

60-"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi najikinga kwako kutokana na kushindwa, na uvivu, na uoga, na

---

[70] Bukhari nambari 634, na Muslim nambari 2707, na tamshi la hadithi liko kwa Muslim ni (Alikuwa Mtume wa Allah rehema na amani ziwe juu yake- akijikinga kutokana na kupatwa na mitihani, na kupatwa na usisuwavu, na makadirio yatakayo muhuzunisha, na kutukanwa na maadui).

[71] Ameitoa hadithi hii Muslim nambari 2720.

[72] Ameitoa hadithi hii Muslim nambari 2721.

ubahili, na ukongwe, na adhabu ya kaburi, Ewe Mwenyezi Mungu ipe nafsi yangu uchamungu, na uitakase kwani wewe ndiye mbora wa kuitakasa, wewe ndiye msimamizi wa nafsi na mtawala wake. Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na elimu isiyo na manufaa, na moyo usiyo nyenyekea, na nafsi isiyo tosheka, na maombi yasiyo jibiwa».[73]

61-"Ewe Mwenyezi Mungu niongoze na unipe msimamo. Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninakuomba uongofu na kupatia».[74]

62-"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi najikinga kwako kutokana na kuondokewa neema zako, na kubadilika kwa afya yako, na kufikiwa ghafla na adhabu zako, na kila aina ya hasira zako" [75].

---

[73] Ameitoa hadithi hii Muslim nambari 2722.

[74] - Ameitoa Hadithii hii Muslim nambari 2725.

[75] Ameitoa Hadithi hii Muslim nambari 2739.

63-"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi najikinga kwako kutokana na shari nilizo zitambua, na kutokana na shari nisizo zitambua"[76].

64-"Ewe Mwenyezi Mungu ziongeze mali zangu, na watoto wangu, na unibariki mimi kwa kile unacho nipa, (78) na refusha maisha yangu juu utiifu wako, na yafanye matendo yangu kuwa mazuri, na nisamehe"[78*77].

---

[76] Ameitoa Hadithi hii Muslim nambari 2716

[77] Inajulishwa na maombi ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake aliyo muombea Anasi (Ewe Mwenyezi Mungu muongezee mali zake, na watoto wake, na mbariki kwa kile ulicho mpa) Ameitoa Hadithi hii Bukhari kwa nambari 1982, na Muslim nambari 660.

[78] Bukhari katika kitabu chake Adabu- Al-Mufrad nambari 653, na ameisahihisha Albaniy katika kitabu silsilat-Al-Ahadithi Al-Sahihi nambari 2241, na katika sahihi Adabu Al-Mufrad ukurasa 244, na yale yaliyo baina ya mabano yanajulishwa na kauli yake Mtume rehema na amani ziwe juu yake alipo ulizwa: Watu gani walio bora? Akasema: "Ni yule umri wake utakuwa mrefu na yakawa mazuri matendo yake" Ameitoa Hadithi hii Tirmidhiy nambari 2329 na Ahmad nambari 17716 na ameisahihisha Albaniy katika sahihi Al-Tirmidhiy 2-271, na hakika nilimuuliza shekhe wetu Ibn Baaz Allah amrehemu kunako kuomba kwa maombi hayo je ni sunnah? Akasema: Ndio.

65-"Hapana Mola apasaye kuabadiwa kwa haki isipokuwa Allah aliye Mtukufu mpole, Hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah Mola mlezi wa Arshi tukufu, Hapana mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah Mola Mlezi wa mbingu na Mola Mlezi wa ardhi, na Mola Mlezi wa Arshi tukufu"[79]

66-"Ewe Mwenyezi Mungu huruma yako naitarajia basi usinijalie ni mwenye kuitegemea nafsi yangu kwa kiasi cha mpepeso wa jicho, na lifanye vizuri jambo langu lote hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa wewe"[80]

---

[79] Bukhari nambari 6345, na Muslim nambar 2730.

[80] Ameipokea Abu Daud nambari 5090, na Ahmad 5-42, na Ameipa daraja la kuwa Hadithi nzuri (Hasan) Albaniy kwenye sahihi Abi Daud 3-25, katika sahihi Adabu-Al-mufrad, 260, na amefanya upokezi wake kuwa mzuri vilevile mwanazuoni Ibn Baaz katika kitabu Tuhfat-Al-Akhbaar ukurasa 24.

67-"Hapana mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa wewe utakasifu ni wako hakika mimi nimekuwa miongoni mwa watu madhalimu"[81]

68-"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ni mja wako mtoto wa mja wako mtoto wa kijakazi wako, nywele zangu za utosi zipo mkononi mwako, hukumu zako kwangu ni zenye kupita, maamuzi yako kwangu ni ya uadilifu, ninakuomba kupitia kila jina lako, ulilo jiita kwalo mwenyewe nafsi yako, au uliloteremsha ndani ya kitabu chako, au umemfundisha yeyote katika viumbe wako, au umelificha ndani ya elimu ya ghaibu iliyo kwako, basi ijaliye Qur'ani ndiyo kitulizo cha moyo wangu na mwangaza wa kifua changu, na kitulizo cha

---

[81] - Tirmidhi nambari 3505, na Al-Hakim na amesahihisha upoekezi wake kuwa ni mauquuf Imam Al-Dhahaby na ameisahihisha Albani katika sahihi Al-Tirmidhi 3-168, na tamshi lake (maombi ya dhaa nuun pindi alipo muomba Allah na yeye akiwa ndani ya tumbo la chewa: An laa ilaha ila anta sub-haanaka inni kuntu mina dhaalimiina) ni kwamba hata omba kwa maombi haya mtu muislamu kabisa kabisa isipokuwa Allah atamjibu maombi yake.

huzuni yangu, na kinacho ondosha msongo wa mawazo yangu"[82]

69-"Ewe Mwenyezi Mungu mwenye kuzigeuza nyoyo geuza nyoyo zetu juu ya utiifu wako"[83]

70-"Ewe Mwenye kuzigeuza nyoyo uthibitishe moyo wangu juu ya dini yako"[84]

71-"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninakuomba yakini na msamaha na afya katika Dunia na Akhera"[85]

---

[82] Ahmad nambar 1-391, 452, Hakim nambari 1-509, na amifanya kuwa Hadithi nzuri (Hasan) Ibn Hajar katika Takhriji Al-Adhkar, na ameisahihisha Albani katika Takhriji Al-Kalami Al-Twayyib ukurasa 73.

[83] Muslim nambari 2654.

[84] Tirimidhi nambari 3522, na Ahmad 4-182, na Hakim 1-525, na 528, ameisahihisha Kuwa ni Hadithi Mauquufu Adhahabiy, na ameisahihisha Albaniy katika sahihi Al-Jaamii, 6-309, na ameisahihisha Tirimidhi 3-171, na alisema Ummu Salamah radhi za Allah ziwe juu yake: Ilikuwa ni zaidi ya maombi yake Mtume rehema na amani ziwe juu yake)

[85] Tirimidhi nambari 3514, na Bukhari katika Adabu-Al-Mufrad nambari 726, na tamshi lake kwa upokezi wa Tirmidhi (Muombe Allah afya katika dunia na akhera) na katika tamshi (Muombeni Allah msamaha na afya hakika mmoja wenu hakupewa baada ya yakini kilicho bora kuliko afya) na ameisahihisha Albani katika sahihi Ibn Majah 3-180 na 3-185, 3-170, na

72"Ewe Mwenyezi Mungu ufanye mzuri mwisho wetu katika mambo yetu yote, na tukinge na udhalili wa dunia na adhabu za akhera"[86]

73-"Mola wangu mlezi nisaidie na wala usinitelekeze, na ninusuru na wala usiniache, na wafanyie vitimbi kwa niaba yangu (maadui zangu), na wala usifanye vitimbi dhidi yangu, na niongoze na ufanye wepesi uongofu kwangu, na ninusuru kwa kila aliye vuka mipaka juu yangu, Mola wangu mlezi nijaaliye niwe ni mwenye kukushukuru, mwenye kukuogopa, mwingi wa utiifu kwako, niwe mwenye kukimbilia kujikurubisha mwenye kujisogeza karibu, Mola wangu mlezi nijaalie niwe mwenye kukubaliwa ninapo tubia, na yatakase madhambi yangu, na niitikie maombi yangu, na thibitisha hoja zangu, na uongoze

---

ina ushahidi, tazama katika Musnad Imam Ahmad kwa upangiliaji wa Ahmad Shaakir, 1-156-157.

[86] Ahmad 4-181, na Twabaraniy katika kitabu Al-Kabiir 2-33 1169, na katika maombi nambari 1436, na Ibn Hibaan nambari 2424, 2425 (Al-Mawaarid) Akasema Al-Haafidh Al-Haythamiy katika Majmaa Al-Zawaid 10-178: Na wapokezi wa Ahmad na moja ya mtiririko wa Twabaraniy ni wakweli)

moyo wangu, na upe msimamo ulimi wangu, na niondoshee husuda ndani ya moyo wangu"[87]

74-"Ewe Mwenyezi Mungu hakika sisi tunakuomba heri alizo kuomba kwazo nabii wako Muhammad -rehema na amani ziwe juu yake- na tunajikinga kwako kutokana na shari alizo jikinga kwako nabii wako Muhammad -rehema na amani ziwe juu yake- na wewe ndiye mwenye kutakwa msaada na juu yako kuna kufikisha, na hapana ujanja wala nguvu isipokuwa ni kwa Mwenyezi Mungu"[88]

75-"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na shari za masikio yangu, na kutokana

---

[87] - Bukhari katika Adabu-Almufrad nambari 664-665, na Abuu Daud nambari 1510-1511, Tirmidhiy nambari 3551, na Ibn Maajah nambari 3830, na Ahmad1-127 na Al-Haakim na amesahihisha kuwa ni hadithi Mauquufu Al-Dhahabiy 1-519, na ameisahihisha Albaniy katika sahihi Abi Daud 1-1414, na katika sahihi Al-Trimidhiy 3-178

[88] Tirmidhiy nambari 3521, na Ibn Maajah nambari 3846 kwa maana yake, na akasema Tirmidhiy: Hadithi hii ni nzuri Ghariibu (Hasanun Gharib) na ameidhohofisha Albaniy katika kitabu Dhaifu Al-Tirmidhiy ukurasa wa 387.

na shari za macho yangu, na shari za ulimi wangu, na shari za moyo wangu, na shari za matamanio yangu"[89]

76-"Ewe Mwenyezi Mungu hakika Mimi najikinga kwako kutokana na ukoma, na mbaranga, na kutokana na maradhi mabaya"[90]

77-"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na tabia mbovu na matendo mabaya, na matamanio mabaya"[91]

78-"Ewe Mwenyezi Mungu hakika wewe ni msamehevu mkarimu unapenda kusamehe basi nisamehe"[92]

---

[89] Abu Daud nambari 1551, na Tirmidhiy nambari 3492, na Nasaai nambar 5470, na wengineo, na ameisahihisha Albaniy katika sahihi Al-Tirmidhiy 3-166, na ameisahihisha Nasaai 3-1108.

[90] - Abu Daud nambar 1554, na Nasaai nambari 5493, na Ahmad 3-192 na ameisahihisha Albaniy katika sahihi Al-Nnasaai 3-1116, na ameisahihisha Al-Tirmidhiy 3-184.

[91] Tirmidhiy nambari 3591, na Ibn Hibaan nambari 2422 (Mawaarid) na Al-Haakim 1/532, na Twabaraaniy katika kitabu Al-Kabiir 36/19/19 na ameisahihisha Albaaniy katika kitabu sahihi Al-Tirmidhiy 3/184.

[92] Tirmidhiy nambari 3513, na Nasaai katika kitabu Al-Kubraa nambari 7712, na ameisahihisha Al-Baaniy katika sahihi Al-Tirmidhiy 3/170

79-"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninakuomba kufanya matendo yenye heri, na kuacha mambo yenye kuchukiza, na kuwapenda masikini, na unifutie madhambi yangu, na unihurumie, na unapo kusudia fitina kwa watu basi nifishe hali ya kuwa si mwenye kufitinishwa, na ninakuomba kukupenda, na kumpenda anaye kupenda, na kupenda matendo yanayo nisogeza kwenye mapenzi yako"[93]

80-"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninakuomba (unipe) kutoka katika heri zote: zile za haraka na za kuchelewa, kwa ninayo yajua na nisiyo yajua, na ninajikinga kwako kutokana na shari zote zinazokuja haraka na zinazochelewa, kwa ninayo yajua na nisiyo yajua. Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninakuomba (unipe) miongoni mwa heri alizo kuomba mja wako na nabii wako, na ninajikinga kwako (uniepushe) na shari

---

[93] Ameitoa Ahmad kwa tamko la Hadithii hii 5/243, na Tirmidhiy nambari 3235 kwa mfano wa Hadithi hii, na ameifanya kuwa ni Hadithi nzuri na akasema: Nimemuuliza Muhammadi Ibn Ismail -anamkusudia Bukhar- akasema: Hadithi hii ni nzuri tena sahihi (Hasanun Sahih) na mwisho wa Hadithi akasema -rehema na amani ziwe juu yake- kuwa hayo ni ukweli basi yafundisheni na mjifunze) Na Al-Haakim 1/521, na ameisahihisha 3/318 Albaaniy katika sahihi Al-Tirmidhiy 3/318.

alizo jikinga kwako mja wako na nabii wako. Ewe Mwenyezi  Mungu hakika mimi ninakuomba pepo, na yaliyo karibu yake miongoni mwa kauli au matendo, na ninajikinga kwako kutokana na moto na yaliyo karibu na moto miongoni mwa kauli au matendo, na ninakuomba ujaalie kila hukumu utakayo hukumu kwangu iwe ni heri"[94]

81-"Ewe Mwenyezi Mungu nihifadhi mimi kwa Uislamu nikiwa nimesimama, nihifadhi mimi kwa Uislamu nikiwa nimeikaa, nihifadhi mimi kwa Uislamu nikiwa nimelala, na usinijaalie kuwa ni mwenye kutukanwa kwa adui au hasidi. Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninakuomba (unipe) kutoka katika kila heri itokayo kwenye hazina ya mkono wako, na ninajikinga

---

[94] Amepokea Abu Daud nambari 3846 kwa tamshi la Hadithi hii, na Ahmad 6/134 na tamshi la ziada la pili limepokelewa kwa mapokeazi yake -Ahmad- Na Haakim amaeisahihisha, na ameikubali Al-Dhahaby 1/521, na tamshi la ziada ya kwanza ni mapokezi yake, na ameisahihisha Albaaniy katika sahihi Ibn Maajah 2/327

kwako kutokana na kila shari itokayo kwenye hazina ya mkono wako"[95]

82-"Ewe Mwenyezi Mungu tugawie sehemu ya kukuogopa kutakako weka kizuizi baina yetu na maasi, na uturuzuku kukutii wewe kutakako tufikisha kuipata pepo yako, na utupe katika yakini itakayo tupunguzia juu yetu matatizo ya dunia. Ewe Mwenyezi Mungu tustareheshe kupitia masikio yetu na macho yetu na nguvu zetu kwa muda ambao utakao tupa uhai, na uvijaalie viwe ni vyenye kubakia, na ujaalie kupata haki zetu kwa aliye tudhulumu, na utunusuru kwa aliye tufanyia uadui, na usijaalie matatizo yetu kuwa katika dini yetu, na usiifanye dunia kuwa ndio jambo muhimu zaidi kwetu, na usiifanye kuwa ndio lengo la mwisho la elimu yetu, na usitusalitishie juu yetu mtu asiye tuhurumia"[96]

---

[95] Al-Haakim 1/525 na ameisahihisha na ameikubali Al-Dhahabiy, na ameifanya kuwa ni Hadithi nzuri (Hasan) Albaniy katika sahihi Al-Jaamii 2/398, na katika silsilatu Al-Ahadithi Al-Sahiihah 4/54 kwa nambari 1540

[96] Tirmidhiy nambari 3502, na Al-Haakim 1/528 na ameisahihisha na ameikubali Adhahabiy na Ibn Sunniy nambari 446, na ameifanya kuwa ni Hadithi nzuri (Hasan) Albaaniy katika sahihi Al-Tirmidhiy 3/168 na katika kitabu Sahihi Al-Jaamii 1/400

83-"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na uoga, na ninajikinga kwako kutokana na ubahili, na ninajikinga kwako kuto rudi kwenye umri wenye udhalili, na ninajikinga kwako kutokana na fitina za dunia na adhabu za kaburi"[97]

84-"Ewe Mwenyezi Mungu nisamehe makosa yangu, na ujinga wangu, na kupituka katika mambo yangu, na kwa yale ambayo wewe wafahamu zaidi yangu. Ewe Mwenyezi Mungu nisamehe mimi mambo ninayo yafanya kwa mzaha, na kwa kukusudia, na makosa yangu, na makusudi yangu, na kila yote yaliyopo kwangu".[98]

85-"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi nimeidhulumu nafsi yangu dhulma nyingi, na hakuna wa kunifutia madhambi isipokuwa wewe, basi nisamehe mimi msamaha utokao kwako, na

[97] Bukhari nambari 2822

[98] Wamekubaliana Hadithi hii Bukhari kwa nambari 6398 na Muslim kwa nambari 2719.

unihurumie hakika wewe mi msamehevu mwengi wa huruma"[99]

86-"Ewe Mwenyezi Mungu kwa ajili yako nimejisalimisha, na kwako nimeamini, na juu yako nimetegemea, na kwako nimejisogeza, na kwa ajili yako napambana. Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi najikinga kwako kwa utukufu wako hapana mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa wewe kuto nipoteza, wewe ndiye uliye hai ambaye hafi, na majini na watu wanakufa"[100]

87-"Ewe Mwenyezi Mungu hakika sisi tunakuomba sababu za kupata huruma yako, na sababu zitakazotia nguvu kupata msamaha wako, na kupata salama kutokana na kila dhambi, na kupata faida kutokana na kila wema, na kufaulu kwa kuipata pepo na kuokoka kutokana na moto"[101]

---

[99] Wamekubaliana juu ya Hadithi hii Bukhari kwa nambari 834, na Muslim nambari 2705.

[100] Wamekubaliana juu Hadithi hii Bukhari kwa nambari 6398, na Muslim kwa nambari 2719.

[101] Al-Haakim 1/525 na ameisahihisha, na ameikubali Al-Dhahabiy, na Al-Baihaqi katika kitabu Al-Daawaat nambari 206, angalia kitabu: Al-

88-"Ewe Mwenyezi Mungu wasamehe waumini wa kiume na wa kike"[102]

89-"Ewe Mwenyezi Mungu nisamehe mimi madhambi yangu, na unipanulie nyumba yangu, na unibariki kwa kile unacho niruzuku"[103]

90-"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninakuomba katika fadhila zako na huruma yako, hakika hakuna anaye miliki hayo isipokuwa wewe"[104]

---

Adhkaar cha imamu Annawawiy ukurasa 340 hakika ameifanya kuwa ni Hadithi nzuri (Hasan) mhakiki Abdul-Qaadir Al-Arnaautu.

[102] Yatokana na Hadithi ya Ubadah -Radhi za Allah ziwe juu yake- amesema: Nimemsikia Mtume wa Allah -rehema na amani ziwe juu yake- anasema: "Atakaye watakia msamaha waumini wanamume na wanawake Allah atamuandikia malipo kwa kila muumini wa kiume na wa kike jema" Amepokea Twabaraany katika kitabu Al-Kabiir 5/202 nambari 5092, na 3/334 na nambari 2155 na ameufanya mtiririko wa mapokezi yake kuwa ni mzuri Al-Haithamy katika kitabu Majmaa Al-zawaaid, 10/210 na amaeifanya vizuri Albaniy katika sahihi Al-Jaamii kwa nambari 5902, 5/242.

[103] Ameitoa Ahmad, 4/64, kwa nambari 16599, na kwa nambari 23114, na kwa nambari 23188, na Tirmidhiy kwa nambari 3500, na wamesema walio kihakiki kitabu Al-musnad, 27/144, na katika 38/197 na katika 38/145: (Hassani lighairihi) na ameifanya kuwa ni Hadithi nzuri kwa kupitia mapokezi mengine) Albaniy katika kitabu sahihi Al-Jaamii 1/399.

91-"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na ukongwe (uzee ulio pindukia), na kuporomoka kutoka sehemu za juu, na kudondokewa na nyumba, na huzuni, na kuzama baharini, na kuungua na moto, na ninajikinga kwako kutochezewa na shetani wakati wa kifo, na ninajikinga kwako nisife kwenye njia yako hali yakuwa ni mwenye kurudi nyumba, na ninajikinga kwako nisife kwa kugongwa na nyoka"[105]

92-"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na njaa, hakika njaa imekuwa ni malazi mabaya, na ninajikinga kwako kutokana na hiyana, hakika hiyana ni rafiki mbaya".[106]

---

[104] Ameitoa Hadithi hii Twabaraniy. Na amesema Al-Haithamiy katika kitabu Majmau Al-zawaaid, 159/10: (wapokezi wake ni wapokezi sahihi isipokuwa Muhammad Ibn Ziad naye ni mkweli) na ameisahihisha Albaniy katika sahihi Al-Jaamii, 404/1, 1278.

[105] Ameitoa Hadithi hii Abu Daud kwa nambari 1552, na Nasaai kwa nambari 5531, na kwa nambari 5532, na ameisahihisha Albaniy katika sahihi Al-Nnasaai, 1123/3, na katika Sahihi sunani Abi Daud 1/425.

[106] Ameitoa Hadithi hii Abu Daud kwa nambari 1547, na Nasaai kwa nambari 5483, na ameisahihisha Albaniy katika kitabu sahihi Al-Nnasaai 1112/3.

93-"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na kushindwa, na uvivu, na uoga, na ubahili, na uzee (ukongwe), na ususuwavu wa moyo, na kughafilika, na umasikini, na udhalili, na umasikini uliyo pindukia, na ninajikinga kwako kutokana na ufakiri, na ukafiri, na uovu, na ugomvi, na unafiki, na (kufanya matendo kwa lengo la kutaka) kusikika kwa watu, na kujionyesha, na ninajikinga kwako kutokana na uziwi, na ububu, na wenda wazimu, na ukoma, na mbaranga, na maradhi mabaya"[107]

94-"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na ufakiri (umasikini ulio pindukia), na uchache, na udhalili, na ninajikinga kwako kuto dhulumu au kudhulumiwa"[108]

---

[107] Ameitoa Hadithi hii Al-Nnasaai kwa nambari 5493, na Haakim 1/530, na ameisahihisha Albaniy katika kitabu sahihi Al-Jaami 406/1, na katika kitabu Irwaai Al-Ghaliil kwa nambari 852.

[108] Ameitoa Hadithi hii Abu Daud kwa nambari 1544, na Al-Nnasaai kwa nambari 5475, na ameisahihisha Albaniy katika kitabu sahihi Al-Nnasaai 1111/3, na katika kitabu sahihi Al-Jaami 407/1, na yaliyo kwenye mabano yamepokelewa kwa Ibn Hibaan(Al-Mawaarid) na ameisahihisha Albani katika sahihi Mawaarid Al-Dhamaan 2/455.

95-"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na jirani muovu katika nyumba ya kudumu, kwani jirani wa kijijini hubadilika"[109]

96-"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na moyo usio kuwa na hofu, na kutokana na maombi yasiyo jibiwa na kutokana na nafsi isiyo tosheka, na kutokana na elimu isiyo na manufaa, na ninajikinga kwako na haya mambo manne"[110]

97-"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na siku mbaya, na usiku mbaya, na wakati mbaya, na rafiki mbaya, na kutokana na jirani mbaya katika nyumba kudumu".[111]

---

[109] Bukhari katika Adabu Al-Mufrad kwa nambari 117, na Haakim 532/1, na ameisahihisha na ameikubali Adhahabi, na ameitoa Hadithi hii Al-Nnasaai kwa nambari 5517, na ameisahihisha Albaniy katika sahihi Al-Jaami 408/1 na ameisahihisha Al-Nnasaai 1118/3.

[110] Ameipokea Hadithi hii Al-Tirmidhi kwa nambari 3482, na Abu Daud kwa nambari 1549, na ameisahihisha Albaniy katika kitabu sahihi Al-Jaami kwa nambari 1295, na ameisahihisha Al-Nnasaai 1113/3.

[111] Ameitoa hadithi hii Al-Twabarani na amesema Al-Haithami katika kitabu Al-Zawaaid 144/10: (na wapokezi wake ni wapokezi sahihi) na ameifanya kuwa ni Hadithi Nzuri Albani katika kitabau sahihi Al-Jaami 411/1, kwa nambari 1290.

98-"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninakuomba pepo, na ninajikinga kwako kutokana na moto) (utasema mara tatu)[112]

99-"Ewe Mwenyezi Mungu nipe ufahamu katika dini"[113]

100-"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninajikinga kwako nisije kukushirikisha kwa jambo ninalolijua, na ninakutaka msamaha kwa nisilolijua"[114]

---

[112] Ameitoa Hadithi hii Al-Tirmidhiy kwa nambari 2572, na Ibn Majah kwa nambari 3340, na Nasaai kwa nambari 5536, na ameisahihisha Albaniy katika kitabu sahihi Al-Tirmidhiy 319/2, na katika kitabu Sahihi Al-Nnasaai 1121/3, na tamshi la Hadithi (Atakaye muomba Allah pepo mara tatu pepo inasema: Ewe Mwenyezi Mungu muingize peponi, na atakaye jikinga kwa Allah kutokana na moto mara tatu moto unasema: Ewe Mwenyezi Mungu mkinge na moto)

[113] Inajulishwa Hadithi hii na upokezi wa Bukhari na Muslim katika maombai ya Mtume -rehema na amani ziwe juu yake- aliyo muombea Ibn Abbas radhi za Allah ziwe juu yake na baba yake. Amepokea Bukhari kwa nambari 143, na Muslim kwa nambari 2477.

[114] Amepokea Hdithi hii Ahmad 403/4, na Ibn Abi Shaibah 10/337, na Al-Twabaraniy katika Muujami Al-Ausatwi 4/284, na ameifanya kuwa ni Hadithi Nzuri Albaniy katika sahihi Al-Targhiib wa Al-Tarheeb,19/1.

101-"Ewe Mwenyezi Mungu ninufaishe kwa uliyo nifundisha, na unifundishe yenye kuwa na manufaa na mimi, na unizidishie elimu"[115]

102-"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninakuomba elimu yenye manufaa, na uniruzuku kilicho kizuri, na matendo yenye kukubalika"[116]

103-"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninakuomba Ewe Allah kwakuwa ni Mmoja wa pekee, Mkusudiwa, Ambaye hakuzaa, wala hakuzaliwa, na hana wakufananishwa na yeyote, unisamehe mimi madhambi yangu, hakika wewe ni msamehevu mrehemevu"[117]

---

[115] Ameitoa Hadithi hii Al-Tirmidhiy kwa nambari 3599, na Ibn Maajah kwa nambari 259, na ameisahihisha Albaniy katika sahihi Ibn Maajah 47/1.

[116] Ameitoa Hadithi hii Ibn Maajah kwa nambari 925, na Al-Nnasaai katika Amali Al-Yaumi wa Al-Lailah kwa nambari 102, na Ahmad 6/294, na 305, na ameisahihisha Albaniy katika kitabu sahihi Ibn Maajah 152/1.

[117] Ameitoa Hadithi hii Al-Nnasaai kwa nambari 1300, na tamshi la Hadithii ni kwa mapokezi yake, na Al-Nnasaai katika Al-Kubraa kwa nambari 7665, na Abu Daud kwa nambari 985, na ameisahihisha Albaniy katika sahihi sunan Al-Nnasaai, 1/147.

104-"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninakuomba kwakuwa sifa ni zako, hapana mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa wewe (uliye mpweke usiye na mshirika) mwenye wema (Ewe) Muumbaji wa Mbingu na Ardhi, Ewe mwenye utukufu na ukarimu, Ewe uliye Hai Ewe uliye simama kwa haki, hakika mimi ninakuomba pepo na ninajikinga kwako kutokana na moto"[118]

105-"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninakuomba kuwa mimi ninakubali kuwa wewe ni Allah hapana mola apasaye kuabudiwa kwa ukweli isipokuwa wewe, uliye wa pekee, mkusudiwa, ambaye hakuzaa, wala hakuzaliwa, na hakuna yeyote wa kufananishwa naye"[119]

---

[118] Amepokea Abu Daud kwa nambari 1495, na Ibn Majah kwa nambari 3858, na Nasaai kwa nambari 1299, na Tirmidhiy kwa nambari 3544, na ameisahihisha Albaniy katika sahihi Al-Nnasai 1/279, na katika sahihi Ibn Majah 2/329.

[119] Abu Daud kwa nambari 985, na Tirmidhy kwa nambari 3475, na Ibn Majah kwa nambari 3857, na Ahmad 360/5, na ameisahihisha Albaniy katika sahihi sunani Al-Tirmidhiy 163/3

106-"Ewe Mola wangu mlezi nisamehe, na nikubalie toba yangu, hakika wewe ni msamehevu mfuta madhambi"[120]

107-"Ewe Mwenyezi Mungu kwa elimu yako ya mambo yaliyo jificha, na kwa uwezo wako juu ya viumbe, nipe uhai kwa kiasi unavyotambua kuwa uhai ni heri kwangu, na unifishe kwa kiasi unavyotambua kuwa kifo ni heri kwangu. Ewe Mwenyezi Mungu, hakika mimi ninakuomba unipe hofu ya kukuogopa kwa wazi na kwa siri, na ninakuomba neno la ukweli katika hali ya kuridhia na hasira, na ninakuomba kuthubutu kwenye hali ya utajiri na umasikini, na ninakuomba neema zisizo malizika, na ninakuomba kitulizo cha jicho kisicho katika, na ninakuomba kuridhia baada ya kupita hukumu, na ninakuomba maisha ya utulivu baada ya kifo, na ninakuomba ladha yakutazama kwenye uso wako, na shauku ya kukutana na wewe, bila ya madhara yenye kudhuru, wala fitina yenye kupoteza.

[120] Abu Daud kwa nambari 1518, na Tirmidhiy kwa nambari 3434, na tamshi ni lake, na Nasai katika Al-Kubraa kwa nambari 10292, na Ibn Majah kwa nambari 3814, na ameisahihisha Albaniy katika sahihi Ibn Majah 321/2, na sahihi Al-Tirmidhiy 153/3.

Ewe Mwenyezi Mungu tupambe kwa pambo la imani, na utujaalie kuwa viongozi wa walioongoka"[121]

108-"Ewe Mwenyezi Mungu niruzuku mapenzi yako, na mapenzi kwa yule ambaye mapenzi yake kwako yataninufaisha kwako. Ewe Mwenyezi Mungu kwa kiasi ulicho niruzuku kutokana na kile ambacho ninakipenda basi kijaalie ni nguvu kwa kile unacho kipenda. Ewe Mwenyezi Mungu kwa kiasi ulicho nikunjulia kwangu mimi basi kijaalie ni faragha kwangu kwa kile unacho kipenda"[122]

109-"Ewe Mwenyezi Mungu nitakase kutokana na madhambi na makosa. Ewe Mwenyezi Mungu nitakase kutokana na madhambi kama jinsi inavyo takaswa nguo nyeupe kutokana na uchafu. Ewe Mwenyezi Mungu, nisafishe kwa theluji na kwa maji ya baridi"[123]

---

[121] Ameipokea Al-Nnasai kwa nambari 1305, na Ahmad 264/4, na ameisahihisha Albaniy katika sahihi Al-Nnasai 280/1 na 1/281.

[122] Ameitoa Al-Tirmidhiy kwa nambari 3491, na ameifanya kuwa ni Hadithi Nzuri, na amesema Shekh Abdul-Qaadir Al-Arnaut (nayo ni kama alivyo sema) angalia uhakiki wake kwenye Jaamii Al-Usuul, 341/4.

[123] Ameitoa Hadithi Hii Muslim kwa nambari 476, na Al- Nnasai kwa nambari 400.

110-"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na ubahili, na uoga, na umri mbaya, na fitina ya kifua, na adhabu za kaburi"[124]

111-Ewe Mwenye Mungu Mola mlezi wa Jibrili, na Mikaeli, na Israfiil, ninajikinga kwako kutokana na joto la moto, na adhabu ya kaburi"[125]

122-"Ewe Mwenyezi Mungu nijaze uongofu, na unikinge na shari ya nafsi yangu"[126]

---

[124] Ameipokea Al-Nnasai kwa nambari 5469 na tamshi lake (Alikuwa Mtume -rehema na amani ziwe juu yake- akijikinga na mambo matano: kutokana na ubahili, na uoga, na umri mbaya, na fitina za kifua, na adhabu za kaburi) Ameitoa Abu Daud kwa nambari 1539, na ameifanya kuwa ni Hadithi nzuri Al-Arnaut katika utoaji wake kwenye kitabu Jaami Al-Usuul 363/4.

[125] Ameitoa Al-Nnasai kwa nambari 1344, na Ahmad 6/61, na Al-Baihaqi katika Al-Daawaat kwa nambari 109, na ameisahihisha Albaniy katika sahihi Al-Nnasai 1121/3, na katika silsilatu Al-Ahadithi Al-Swahihah kwa nambari 1544.

[126] Ameipokea Al-Tirmidhiy na tamshi lake 5/519 kwa nambari 3483, na ameitoa Ahmad 23/197 kwa nambari 19992, na Al-Haakim 1/510 kwa mfano wake vile vile, na wamesema wahakiki wa mtiririko wa mapokezi kunako hadithi hii kwa Ahmad 33/197) Mtiririko wake ni sahihi kwa masharti ya Bukhar na Muslim) na kuhusu tamshi la Tirmidhiy ameidhoofisha Albaniy karika Dhaifu Al-Tirmidhiy ukurasa wa 379.

113-"Ewe Mwenye Mungu hakika mimi ninakuomba elimu yenye manufaa, na ninajikinga kwako kutokana na elimu isiyo na manufaa".[127]

114-"Ewe Mwenyezi Mungu mola mlezi wa mbingu (saba) na mola mlezi wa ardhi, na mola mlezi wa Arshi tukufu, mola wetu mlezi na mola mlezi wa kila kitu, mwenye kupasua mbegu na kokwa, na mwenye kuteremsha taurati na injili na Qur'ani, ninajikinga kwako kutokana na shari ya kila kitu wewe ni mwenye kukishika kwa nywele za utoshi. Ewe Mwenyezi Mungu wewe ndiye wa mwanzo hakuna kitu kabla yako, na wewe ndiye wa mwisho hakuna kitu baada yako, na wewe ni wa wazi hakuna kitu juu yako, na wewe ni wa ndani hakuna kitu chini yako, tulipie madeni na ututosheleze kutokana na ufakiri"[128]

---

[127] Ameitoa Al-Nnasai katika kitabu Al-Kubraa kwa nambari 7867, na Ibn Majah kwa Nambari 3843 na ameifanya kuwa ni Hadithi Nzuri Albaniy katika sahihi sunan Ibn Majah 327/2, na tamshi lake (Muombeni Allah elimu yenye manufaa na mjikinge kwa Allah kutokana na elimu isiyo kuwa na manufaa).

[128] Ameitoa Muslim kwa nambari 2713, kutoka kwa Abi Hurairah -Radhi za Allah ziwe Juu yake-

115-"Ewe Mwenyezi Mungu unganisha baina ya nyoyo zetu, na tengeneza baina yetu, na tuongoze njia ya amani, na tuokoe kutoka kwenye kiza kwenda kwenye mwanga, na tukinge kutokana na uchafu unao onekana na usio onekana, na utubariki sisi katika usikivu wetu, na kuona kwetu, na mioyo yetu, na wake zetu, na vizazi vyetu, na tusamehe hakika wewe ni msamehevu mrehemevu, na tujaalie ni wenye kushukuru neema zako wenye kusifia neema hizo juu yako, wenye kuzipokea, na tutimizie juu yetu"[129]

116-"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninakuomba mambo ya heri, na maombi ya heri, na heri ya kufaulu, na heri ya matendo, na heri ya kutubia, na heri ya maisha, na heri ya kifo, na unithibitishe, na itie uzito mizani yangu, na uihakiki imani yangu, na linyanyue daraja langu, na unikubalie swala zangu, na unisamehe makosa yangu, na ninakuomba daraja za juu peponi. Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninakuomba ufunguzi wa heri, na mwisho wake, na

---

[129] Ameitoa Hadithi hii Abu Daud kwa nambari 969, na Haakim na tamshi lake 1/265, na amesema: (Sahihi kwa masharti ya Muslim) Na ameikubali Adhahaby 26/1, na ameisahihisha Albaniy katika sahihi Adabu Almufrad kwa nambari 630.

mkusanyiko wake, na mwanzo wake, na uwazi wake,na undani wake,

na daraja za juu peponi amiin. Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninakuomba heri zenye kuja, na heri za ninayofanya, na heri ninazotenda, na heri za ndani, na heri za nje, na daraja za juu peponi amiin. Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninakuomba unyanyue utajo wangu, na uniondolee makosa yangu, na ulifanye vizuri jambo langu, na uusafishe moyo wangu, na uihifadhi tupu yangu, na utie mwangaza moyo wangu, na unisamehe dhambi zangu, na ninakuomba daraja za juu peponi amiin. Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninakuomba utie baraka ndani ya nafsi yangu, na ndani ya masikio yangu, na ndani ya macho yangu, na ndani ya roho yangu, na ndani ya maumbile yangu, na ndani ya tabia yangu, na kwa watu wangu, na ndani ya uhai wangu, na ndani ya kifo changu, na ndani ya matendo yangu, nikubalie mema yangu, na ninakuomba daraja za juu peponi amiin"[130]

---

[130] Ameitoa Hadithi hii Al-Haakim kutoka kwa Ummu Salamah Marfu'u (hali ya kunyanyuliwa mpaka kwa Mtume -rehema na amani ziwe juu yake-) 1/520 na ameisahihisha na ameikubali Adhahabiy 520/1, na Al-

117-"Ewe Mwenyezi Mungu niepushe na tabia mbovu, na matamanio mabaya, na matendo machafu, na maradhi yenye kuchukiza".[131]

118-"Ewe Mwenyezi Mungu nikinaishe kwa kile unacho niruzuku, na unibariki ndani yake, na unipe badala kwa kila kinachopotea kwangu kilicho kuwa heri" [132]

119-"Ewe Mwenyezi Mungu nihesabu mimi hesabu nyepesi"[133]

---

Baihaqi katika kitabu Al-Dawaat kwa nambari 225, na Al-Tabarany katika kitabu Al-Kubraa 23/326, kwa nambari 717.

[131] Ameitoa Haakim 1/523 na amesema:(sahihi kwa sharti la Muslim) na ameikubali Adhahaby 532/1, na ameitoa Al-Tabarany katika Al-Muujam Al-Kubraa 19/19 kwa nambari 36, na ameisahihisha Albaniy katika Dhwilaal Al-Jannah kwa nambari 13.

[132] Ameitoa Al-Haakim 1/532 na ameisahihisha na ameikubali Adhahabiy 510/1, kutoka kwa Ibn Abas -Radhi za Allah ziwe juu yao, na Al-Baihaqi katika kitabu Al-Aadab kwa nambari 1084, na katika Al-Daawaat Al-Kubraa 211, na ameifanya kuwa ni Hadithi Nzuri Al-Haafidh Ibn Hajar katika Al-Futhaat Al-Rabaaniyyah 4/383.

[133] Ameipokea Ahmad 48/6, na Al-Haakim 1/255, na amesema: (sahihi kwa sharti la Muslim) na ameikubali Adhahabiy 255/1, Amesema Ummu Aisha -Radhi za Allah ziwe juu yake-: pindi alipo ondoka nikasema: Ewe

120-"Ewe Mwenyezi Mungu nisaidie juu ya kukutaja, na kukushukuru, na kuwa miongoni mwa waja wako wema"[134]

121"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninakuomba imani isiyo tetereka, na kuwa karibu na Mtume Muhammadi -rehema na amani ziwe juu yake- ndani ya pepo za juu zenye kubakia milele"[135]

---

Nabii wa Allah ni ipi hesabu iliyo nyepesi?Akasema: "Ni Allah atazame ndani ya kitabu cha mja kisha amsamehe, na hakika atakaye hojiwa hesabu siku hiyo ewe Aisha ataangamia, na kila kinacho mpata muumini Allah- aliye tukuka na kutakasika- ni mwenye kumfutia miongoni mwa makosa yake hata mwiba unao mchoma" Na akasema kunako Hadithi hii mwanachuoni Albaniy katika Mishkaat Al-Misbaahi (Mtiririko wa mapokezi yake ni mzuri).

[134] Ameitoa Ahmad 2/299, na Al-Haakim 499/1, na ameisahihisha, na ameikubali Adhahabiy, na hadithi hii ni kama walivyo sema, kuwa ipo kwa Abuu Daud kwa nambari 1524, na Al-Nnasaai katika kitabu Al-Kubraa kwa nambari 9973, na ameisahihisha Albaniy katika sahihi Al-Aadabu Al-Mufrad kwa nambari 534.

[135] Ameitoa Ibn Hibaan (Almawaarid) ukurasa wa 604, kwa nambari 2436 kutoka kwa Ibn Masoud -Radhi za Allah ziwe juu yake- mapokezi yake yakiishia kwake, na amepokea Ahmad kutoka katika mapokezi mengine 386/1,400, na Nasai katika kitabu Amalu Al-yaumi walailah kwa nambari 869 na ameifanya kuwa ni Hadithi nzuri mwanazuoni Albaniy katika Asilsilati Al-Sahiihah chini ya nambari 2301..

122-"Ewe Mwenyezi Mungu nikinge na shari za nafsi yangu, na nipe maazimio juu ya uongofu wa jambo langu. Ewe Mwenyezi Mungu nisamehe makosa niliyo yafanya kwa siri, na niliyo yafanya kwa wazi, na niliyo yakosea, na niliyo yakusudia, na niliyo yatambua, na nisiyo yatambua"[136]

123-"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na kushindwa kulipa deni, na kushindwa na maadui, na kutukanwa na maadui".[137]

124-"Ewe Mwenyezi Mungu nisamehe, na uniongoze, na uniruzuku, na unipe afya, na ninajikinga

---

[136] Ameitoa Al-Nnasai katika kitabu Al-Kubraa 6/246 kwa nambari 10830, na Al-Haakim 510/1 na ameisahihisha, na ameikubali Adhahabiy, na ameitoa Ahmad 444/4, na Al-Musnad Al-Muhaqaq,33/197, na nambari 19992, na amesema Al-Hafidh katika kitabu Al-Iswaabah (Mtiririko wa mapokezi yake ni sahihi) Na ameisahihisha Albaniy katika kitabu Takhiriiji riyadhi Al-Swaalihiina, na katika kuielezea Hadithi nambari 1495.

[137] Ameitoa Al-Nnasai kwa nambari 5475, na Ahmad 2/173, na ameisahihisha Albaniy katika Sahihi Al-Nnasai 1113/3.

kwako kutokana na ufinyu wa kisimamo siku ya kiyama" (139)[138]

125-"Ewe Mwenyezi Mungu nistareheshe kwa usikivu wangu, na kuona kwangu, na yajaalie macho na masikio ni vyenye kubakia kwangu, na ninusuru juu ya atakaye nidhulumu, na chukua kutoka kwake haki zangu"[139]

126-"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninakuomba maisha yaliyo bora, na kifo kilicho kati na kati, na marejeo ya Akhera yasiyo huzunisha wala kufedhehesha"

127-"Ewe Mwenyezi Mungu sifa zote ni zako. Ewe Mwenyezi Mungu hakuna wa kuzuia ulicho kitoa, wala hakuna wa kutoa ulicho kizuia, wala hakuna wa kumuongoza uliye mpoteza, wala hakuna wa

---

[138] Ameipokea Al-Nnasai kwa nambari 1617, na Ibn Majah kwa nambari 1356, na ameisahihisha Albaniy katika Sahihi sunan Al-Nnasai 356/1, na katika sahihi Ibn Majah, 226/1.

[139] Ameitoa Al-Tirmidhiy kwa nambari 3681, na Bukhari katika Adabu Al-Mufrad kwa nambari 650 na Al-Hakim 1/523, na ameisahihisha na ameikubali Adhahabiy, na ameifanya kuwa ni Hadithi nzuri Albaniy katika sahihi Al-Tirmidhiy 188/3.

kumpoteza uliye muongoza, wala hakuna wa kutoa kwa kile ulicho kizuia, wala hakuna wa kuzuia kwa kile ulichokitoa, na wala hakuna wakumuweka karibu uliye muweka mbali, na wala hakuna wa kumuweka mbali uliye muweka karibu. Ewe Mwenyezi Mungu tukunjulie baraka zako juu yetu, na rehema zako, na fadhila zako, na riziki zako. Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninakuomba neema zenye kubakia ambazo hazina kizuizi wala kuondoka. Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninakuomba neema siku za umasikini, na amani siku za hofu. Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ni mwenye kujikinga kwako kutokana na shari ulizo tupa na shari ulizo zizuia. Ewe Mwenyezi Mungu tupendelee imani na uipambe kwenye mioyo yetu, na uchukize kwetu ukafiri na uovu na kufanya makosa, na utujaalie miongoni mwa walio ongoka. Ewe Mwenyezi Mungu tufishe tukiwa ni waislamu, na tupe uhai tukiwa ni waislamu, na tukutanishe na waja wema bila ya udhalili wala kufitinishwa. Ewe Mwenyezi Mungu wapige vita makafiri wanao wapinga mitume wako, na wanao zuia njia yako, na jaalia juu yao maangamivu yako ya adhabu zako. Ewe Mwenyezi Mungu wapige vita

makafiri wale walio pewa vitabu, wewe ndiye Mungu wa kweli" (Ameen)[140].

128-"Ewe Mwenyezi Mungu nisamehe, na unihurumie, na uniongoze, na unipe afya, na uniruzuku"[141]

"....na litengeneze na ulifanye vizuri jambo langu, na uninyanyue"[142]

---

[140] Ameipokea Ahmad kwa matamshi ya hadithi hii, 3/424 na 24/246, kwa nambari 15492, na yaliyo kwenye mabano ni upokezi wa Al-Haakim 1/507,3/23-24, na ameitoa Bukhari katika kitabu Adabu Al-Mufrad kwa nambari 699, na ameisahihisha Albaniy katika Takhriji fiqh Al-Siirah ukurasa 284, na katika sahihi Adabu Al-Mufrad cha Bukhari kwa nambari 538 ukurasa 259, na wamesema wanao fanya uhakiki wa Musnadi 24/246: wapokezi wake ni wakweli)

[141] Ameipokea Muslim kwa nambari 2696, na kwa nambari 2697, na katika upokezi wa Muslim: (Hakika maneno hayo yanaikusanya dunia yako na Akhera yako) na katika Sunan Abi Daud kwa nambari 850: Amesema: (pindi alipoondoka yule Bedui akasema Mtume -rehema na amani ziwe juu yake: "Hakika ameijaza heri mikono yake".

[142] Tazama: Al-Tirmidhiy kwa nambari 284, na Ibn Majah kwa nambari 898, na ameisahihisha Albaniy katika sahihi Ibn Majah 1/148, na ameisahihisha Al-Tirmidhiy 1/90.

129-"Ewe Mwenyezi Mungu tuzidishie wala usitupunguzie, na utukirimu na wala usitudhalilishe, na utupe na wala usitunyime, na utupe haki zetu na wala usizitoe haki zetu juu yetu, na uturidhie na uridhie juu yetu"[143]

130-"Ewe Mwenyezi Mungu kama ulivyo fanya vizuri maumbile yangu basi ifanye kuwa nzuri tabia yangu"[144]

131-"Ewe Mwenyezi Mungu niwezeshe na unijaalie kuwa muongofu aliyeongozwa"[145]

132-"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninakuomba uwezo katika mambo, na kukusudia juu ya

---

[143] Al-Tirmidhiy 5/326 kwa nambari 3173, na Al-Haakim 2/98, na ameisahihisha, na ameifanya kuwa ni Hadithi nzuri Abdul Qaadir Al-Arnautu katika uhakiki wake kwenye kitabu Jaamii Al-Usuul 11/282 kwa nambari 8847.

[144] Ameitoa Ahmad 68/6, na 155, na 403/1 na Ibn Hibaan (2423-Mawaarid) Wa Al-Twayaalisiy 374, na Musnad Abi Yaalaa kwa nambari 5075, na ameisahihisha Albaniy katika Irwaai Al-Ghaliil 115/1, kwa nambari 74.

[145] Imejulishwa juu maombi haya maombi ya Mtume -rehema na amani ziwe juu yake-kwa Jariri -Radhi za Allah ziwe juu yake-angalia: Bukhari kwa nambari 6333, na vile vile kwa nambari 3020,3036, na nyinginezo.

uongofu, na ninakuomba matendo na sifa zitakazokuwa ni sababu ya kupata rehema zako, na matendo yatakayo tilia nguvu kupata msamaha wako, na ninakuomba kushukuru neema zako, na uzuri wa kukuabudu wewe, na ninakuomba moyo ulio salimika, na ulimi unao sema kweli, na ninakuomba heri unazo zitambua, na ninajikinga kwako kutokana na shari unazo zitambua, na ninakutaka msamaha kwa unayo yajua, hakika wewe ni mjuzi wa mambo yaliyo fichikana"[146]

---

[146] Ameipokea Ahmad 28/338, kwa nambari 17114, na 28/356, kwa nambari 17133, na Tirmidhiy kwa nambari 3407, na Al-Tabarany katika kitabu Al-Muujamu Al-Kubraa kwa tamshi la Hadithi hii kwa nambari 7135, na kwa nambari 7157, na 7175, na kwa nambari 7176, na 7177, na 7178, na 7179, na 7180, na ameitoa Ibn Hibaan katika sahihi yake 3/215 kwa nambari 935, na 5/310, kwa nambari 1974, na ameifanya kuwa ni Hadithi Nzuri Shaibu Al-Arnautu katika sahihi Ibn Hibaan, 5/312, na ameifanya kuwa ni Hadithi nzuri kwa njia yake wahakiki wa Musnad, 28/338, na ameitaja Albaniy katika Silsilati Al-Ahaadithi Al-Sahihih katika juzuu ya saba, kwa nambari 3228, na katika Mawaarid Al-Dhamaan kwa nambari 2416, na 2418, na amesema: (Sahihi kwa upokezi mwingine)

133-"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninakuomba Pepo ya Firdausi (ambayo) ndio pepo ya juu zaidi[147]

134-"Ewe Mwenyezi Mungu ifanye upya imani ndani ya moyo wangu"[148]

135-"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na swala isiyo kuwa na manufaa"[149]

---

[147] Imechukuliwa kutokana na kauli ya Mtume -rehema na amani ziwe juu yake-(...mtakapo muomba Allah basi muombeni pepo ya Firdausi, hakika pepo hiyo ndio pepo ya kati na kati, na ndio pepo ya juu zaidi, na juu yake ndiko kuna Arshi ya Mwenyezi Mungu, nako ndiko itokapo mito ya pepo) Ameipokea Bukhari kwa nambari 2790, na nambari 7423.

[148] Imechukuliwa kutoka kwenye Hadithi ya Abdullahi Ibn Omar -Radhi za Allah ziwe juu yao- amesema: Amesema Mtume -rehema na amani ziwe juu yake-: "Hakika imani inafubaa ndani ya moyo wa mmoja wenu kama jinsi nguo inavyo fubaa, basi muombeni Allah azifanye upya imani ndani ya mioyo yenu" Ameipokea Hakim 1/4, na ameisahihisha na ameikubali Adhahabiy, na amesema Al-Haithamiy katika Majmai Al-Zawaaid 1/52: (Amepokea Al-Tabaraaniy katika kitabu Al-Kabiir, na mtiririko wa mapokezi yake ni mzuri) na Ameifanya kuwa ni Hadithi Nzuri Albaniy katika Silsilati Al-Ahaadithi Al-Sahihih, 4/113, kwa nambari 1585.

[149] Abu Daud kwa nambari 1549, na ameisahihisha Albaniy katika sahihi sunan Abi Daud 1/424.

136-"Ewe Allah hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na jirani mbaya, na mke atakaye nitoa mvi kabla ya uzee, na kutokana na mtoto atakaye kuwa bwana juu yangu, na kutokana na mali zitakazokuwa ni adhabu juu yangu, na kutokana na rafiki mwenye vitimbi jicho lake likiniona kama rafiki, na moyo wake ukinisubiri kwa kunifanyia maudhi, akiona jema analifunika, na akiona ovu analitangaza"[150]

137-"Ewe Mwenyezi Mungu usinihuzunishe siku ya kiyama"[151]

138-"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninakuomba kusamehewa Duniani na Akhera"[152]

---

[150] Ameipokea Al-Tabaraani katika kitabu Al-Duaa, 3/1425 kwa nambari 1339, na akasema Albaniy katika silsilat Al-Ahaadith Al-Sahihih 7/377 kwa nambari 3137:(nimesema: Na upokezi huu ni mzuri, wapokezi wake wote wanatokana na wapokezi wa kitabu cha Al-Tahdhibi..)

[151] Ameipokea Ahmad 29/596, kwa nambari 18056, na wamesema wanao hakiki Musnad: (mapokezi yake ni sahihi), na amaeitoa Al-Twabaraaniy katika Al-Muujam Al-Kabiir, 3/20, kwa nambari 2524 kwa tamshi lake: ((Ewe Mwenyezi Mungu usinihuzunishe siku ya kiyama, na wala usinihuzunishe siku yenye ubaya).

139-"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na elimu isiyofaa, na matendo yasiyo pandishwa, na moyo usio na hofu, na kauli isiyo sikika"[153]

140-"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na msongo wa mawazo na huzuni, na kushindwa, na uvivu, na ubahili na uoga, na ugumu wa madeni, na kudhulumiwa na watu"[154]

141-"Ewe Allah hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na adhabu ya moto, na ninajikinga kwako kutoka na adhabu za kaburi, na ninajikinga kwako kutokana na fitina zenye kuonekana na zisizo onekana,

---

[152] Ameipokea Ibn Maaja kwa nambari 3851, na ameisahihisha Albaniy katika sahihi Ibn Majah 3/259, na katika silsilah Al-Ahaadithi Al-Sahihih kwa nambari 1138.

[153] Ameitoa Ibn Hibaan kwa nambari 2440 (Mawaarid) na ameisahihisha Albani katika sahihi Mawaarid Al-Dhwamaan, 2/454, kwa nambari 2066.

[154] Ameipokea Bukhari kwa nambari 6363 amesema Anas: (Nilikuwa nikimtumikia Mtume wa Allah -rehema na amani ziwe juu yake- kila mara anapoteremka, nilikuwa nikimsikia anasema mara nyingi: "Ewe Allah hakika mimi ninajikinga kwako..."

na ninajikinga kwako kutokana na fitina za Masihi Dajal"[155]

142-"Ewe Allah hakika mimi ninakuomba kufa shahidi katika njia yako".[156]

143-"Ewe Allah nisamehe. Ewe Allah nijaalie siku ya kiyama niwe juu zaidi ya waja wako miongoni mwa watu. Ewe Allah, nisamehe makosa yangu, na uniiingize siku ya kiyama kuingia kuzuri".[157]

144-"Ewe Mwenyezi Mungu niongoze miongoni mwa ulio waongoza, na unisamehe miongoni mwa waliosamehewa, na unitawalishe miongoni mwa ulio

---

155 Ameipokea Muslim kwa nambari 2867, na ndani yake (jilindeni kwa Allah kutokana na adhabu za moto....) (jilindeni kwa Allah kutokana na adhabu za kaburi...) mpaka mwisho wake.

156 Ameipokea Muslim kwa nambari 1909, na yaliyo kwenye mabano yanatokana na kauli yake Mtume -rehema na amani ziwe juu yake-: "Atakaye muomba Allah kufa shahidi kwa ukweli Allah atamfikisha daraja za mashahidi, hata kama atakufa akiwa juu ya kitanda chake).

157 Ameipokea Bukhari kwa nambari 4323, na Muslim kwa nambari 2498, nayo imenyambuliwa kutoka kwenye maombi ya Mtum -rehema na amani ziwe juu yake- kwa Ubeid Abi Amir, na kutokana na maombi yake- rehema na amani ziwe juu yake- kwa Abuu Burdah Radhi za Allah ziwe juu yao.

watawalisha, na unibariki kwa kile ulicho nipa, na unikinge na shari ulizo zipitisha, kwani hato dhalilika uliye muweka karibu, umetukuka Mola wetu Mlezi na umetakasika".[158]

145-"Mola wangu Mlezi nisamehe makosa yangu siku ya kiyama"[159]

146-"Ninamuomba Allah Mtukufu anifutie madhambi yangu, ambaye hakuna mola aabudiwaye kwa haki isipokuwa yeye, Mwenye uhai uliokamilika na

---

[158] Ameipokea Ahmad katika Musnad 3/249 kwa nambari 1723, na wamesema wahakiki wa Musnad 3/249: (mapokezi yake ni sahihi), na upokezi huu ni wa moja kwa moja bila kuifungamanisha na sala ya witri kama jinsi ilivyokuja katika mapokezi mengine, na katika upokezi huu amesema Anas -Radhi za Allah ziwe juu yake-: (Alikuwa Mtume akitufundisha maombi haya...)

[159] Ameipokea Muslim kwa nambari 214, palisemwa kwa Mtume -rehema na amani ziwe juu yake- Ewe Mtume wa Allah, hakika Ibn Jadaan alikuwa katika zama za ujinga akiunganisha udugu, na akilishiza masikini, je hayo yatamnufaisha? Akasema: "Hapana, hakika yeye hakusema hata siku moja Mola wangu Mlezi nisamehe makosa yangu siku ya kiyama".

usimamizi wake wa kusimamia viumbe wote, na nina omba msamaha kwake"[160].

147-"Ewe Mwenyezi Mungu nisamehe makosa yangu, na niondoshee chuki ndani ya moyo wangu, na unikinge kutokana na fitina zenye kupotosha"[161]

---

[160] Ameipokea Al-Tirmidhy kwa nambari 3577, na ameisahihisha Albani katika sahihi Al-Tirmidhiy 3/469: (Atakaye sema maneno hayo Allah atamsamehe hata kama alikimbia siku ya vitani)

[161] Imechukuliwa kutoka katika maombi ya Mtume -rehema na amani ziwe juu yake-kwa Aisha- Radhi za Allah ziwe juu yake-(Ewe Allah msamehe makosa yake, na muondoshee chuki ndani ya moyo wake, na mkinge na fitina zenye kupoteza) Ameitoa Ibn Asaakir kwa mapokezi yake katika (Al-Arbauna fii manaaqib ummahaat Al-Muuminina) ukurasa wa 85 kutoka kwa Aisha -Radhi za Allah ziwe juu yake, amesema:(Hadithi hii ni sahihi nzuri, kutokana na hadithi ya Baqiyah Ibn Al-Waliid), na ameitoa Ibn Al-Suniyyi kwa mfano wake katika Amalu Al-Yaumi walailah, kwa nambari 457, na katika karatasi nyingine za Ibn Suniyyi amesema: (Na unikinge na shetani) badala ya (kutokana na fitina zenye kupotosha), anagalia utokaji wake kwa Albani katika kitabu Al-Dhaifu kwa nambari 4207, na hadithi hii inatiliwa nguvu kwa ushuhuda kutoka kwa ummu Salamah -Radhi za Allah ziwe juu yake- inapatikana kwa Ahmad kwa nambari 6/265,44/2 kwa mfano wake, na tamshi lake (Sema Ewe Mwenyezi Mungu Mola mlezi wa Nabii Muhammadi nisamehe makosa yangu, na uniondoshee chuki ndani ya moyo wangu, na unikinge kutokana na fitina zenye kupotosha kwa wote utakao tuweka hai) na ameifanya kuwa ni hadithi nzuri Al-Haithamy katika Majmau Al-Zawaaid 10/27 nayo ipo kwa Tabaraan katika Al-

148-"Ewe Allah nibakize maisha yangu yote nikiwa katika kufuata mwendo wa Nabii wako -rehema na amani ziwe juu yake- na unifishe nikiwa juu ya utaratibu wake, na unikinge kutokana na fitina zenye kupotosha"[162]

149-"Ewe Allah shusha rehema juu ya Muhammad na wafuasi wake Muhammad kama ulivyo shusha rehema

---

Muujam Al-Kabiir 23/388 kwa nambari 785 bila ya matamshi yake: (kwa muda wote utakao tuweka hai) na hadithi hii ina ushahidi kutokana na hadithi ya ummu haanii -Radhi za Allah ziwe juu yake- amesema: Ewe Mtume wa Allah nifundishe maombi nitakayo kuwa nikiomba, akasema: (Sema Ewe Allah, nisamehe makosa yangu..) Hadithi hii ameitoa Al-Kharaaitwii katika kitabu Ighitilaal Al-Quluub kwa nambari 52, na katika Masaawi Al-A khlaaq kwa namba 323.

[162] Ameitoa Al-Baihaq katika Al-Kubraa, 5/95 kutokana na maombi ya Ibn Omar ikiwa ni maombi yaliyo simamia kwake, na amenukuu hayo Ibn Al-Mulaqan katika kitabu Al-Badiri Al-Muniir 6/309, na amesema hali ya kunukuu kutoka katika kitabu Al- Dhiyaai:(mapokezi yake ni mazuri) na amesema Ibn Masoud -Radhi za Allah ziwe juu yake-(Asiseme mmoja wenu: Ewe Allah hakika mimi ninajikinga kwako kutokana na fitina, hakuna yeyote isipokuwa anakuwa amefungamana na fitina, kwakuwa Allah anasema: "Hakika ya mali zenu na watoto wenu ni fitina" (Surah Taghabun:15) basi yeyote atakaye jikinga basi ajikinge kwa Allah kutokana na fitina zenye kupotosha) Ameitoa Ibn Jarir, katika Tafsiri yake,13/475 kwa namabri 15912, na ameitaja ibn Batwaal katika ufafanuzi wake juu ya sahihi Al-Bukhari, 4/13.

juu ya Ibrahim na wafuasi wa Ibrahim hakika wewe ni mwenye sifa tukufu, na shusha baraka juu ya Muhammad na wafuasi wa Muhammad kama ulivyo shusha baraka juu ya Ibrahim na wafuasi wa Ibrahim hakika wewe ni mwenye sifa tukufu".[163]

Na kila sifa njema ni zake Allah Mola Mlezi wa viumbe, kama inavyotakikana kwa utukufu wake, na ukubwa wa utawala wake. Ewe Allah teremsha rehema na amani juu ya Nabii wetu Muhammad na juu ya watu wake, na sahaba zake, na walio mfuata kwa wema mpaka siku ya Kiyama.

[163] Ameipokea Bukhari kwa nambari 3370, na yaliyo baina ya mabano yanatokana na Hadithi ya Abuu Huraira -Radhi za Allah ziwe juu yake- inapatika kwa Muslim kwa nambari 405..

# Index


Maombi kutoka kwenye Qur'ani na Sunna .................. 3

Utangulizi ........................................................... 7

Ubora (fadhila) za maombi ........................................ 9

Maombi kupitia Qur'ani na Sunna ............................. 18